

NENO LA MUNGU

LISILOBADILIKA



Mnaweza kuketi. Tunashukuru sana kwamba Bwana mwema ametupa jioni tulivu kwa ajili ya ibada hii. Hali ya hewa yenye mawingu, ikibashiri mvua ya ngurumo usiku wa leo, na ni jioni nzuri, yenye baridi, tunamshukuru Bwana kwa hiyo.

² Ninashukuru sana kwa yale Bwana wetu amefanya katika mkutano huu mdogo, wa siku tano hapa Lakeport, na kwa ajili ya ushirika mzuri ambao tumefurahia pamoja na marafiki zangu, wenzangu, na mimi mwenyewe, ushirikiano wenu mwema, upendo wenu, zawadi zenu, msaada wenu. Kwa urahisi hatuna maneno ya kuelezea yale tunayowazia kulihusu.

³ Nami niliwauliza hao wavulana nilipokuwa nikiingia, mabawabu walikuwa huko nje upande wa nyuma, walikuwa wakihesabu ma—matoleo ya jioni, nami niliwauliza tu, ili nijue kwa hakika, kama kulikuwa na fedha za kutosha kulipia bili zote, nao wakasema kulikuwako, kwa hiyo asanteni sana kwa msaada wenu. Kisha wakasema kulisalia za kutosha hata wakaweka sadaka ya upendo kwa ajili ya misheni ya kigeni. Mungu awabariki kwa hilo.

⁴ Siku moja, huenda msilione hapa, lakini siku moja, katika ile Nchi nyingine, mtaona, kama Mungu akinisaidia kurudi ng'ambo, hao watu waliookoka watahesabiwa kwenu. Labda hujaitwa kwenda, lakini unaweza kumsaidia mtu aliyeitwa kwenda, na pamoja thawabu zitagawanwa Utukufuni.

⁵ Na mnapoona Huko, kama nilivyoona lile ono, na kuona ya kwamba, hao watu wanakuja kwako, na ambako vitu vyote vimefanywa kamilifu, wanakukumbatia, wakisema, “Ndugu mpendwa, kama usingesaidia usiku huo katika ile mikutano, Ndugu Branham hangalienda, nami nisingaliokoka, lakini kwa sababu ulisaidia!” Sasa, pesa zingekufaa nini Huko? Unaona?

⁶ Kwa hiyo, najua ni kujitolea, kwe—kweli ndivyo, kwa sababu nyakati si nzuri kama zilivyokuwa. Lakini—lakini nawaambia marafiki, laiti mngaliweza tu kuona hali za nchi za ng'ambo! Kila Mmarekani, haidhuru kama yeye ni ombaomba mtaani, yeye ni milionea ukilinganisha na baadhi ya watu hao walivyo. Kamwe hamtambui jinsi watu hao walivyo maskini huko India, na kote, wao ndio fukara sana *kuliko* wote.

⁷ Ninapoenda huko jioni moja na kuwaona wakiwabeba watu hao kwenye hizo, kitu cheupe tu, shuka au turubai lililotupwa juu yao, wanawapeleka kwenye tanuru kubwa na kuwatupa ndani, hawajui wao ni akina nani, walifia tu mtaani, ombaomba.

Wala hakuna Yohana 14, na *Ng'ambo Ya Pili*, na nyimbo nzuri zilizoiimbwa, na maua, na ibada za mazishi, la, kwa urahisi ndiyo njia bora tu wanayoweza, kuchoma maiti, kuwaondoa, hivyo tu. Kwa hiyo, watu hao ni watu ambao Yesu aliwafia, nao wana haki ya kumjua Mungu kama tu tulivyo nayo sisi.

⁸ Ninapokuja nyumbani na kuangalia kote na kuona makanisa makubwa, mazuri na—na watu waliovalia nadhifu, na—nasi... halafu ninaenda kule na kuangalia kote, ninawaona maskini jamaa hao wamelala pale wakifa kwa njaa, na hata kamwe hawakujua kulikuwa na Mungu. Nawe unasema, “Mungu...” wanasema, “Mungu yupi?” Maelfu yao, mwajua, kwa hiyo hawajui. Halafu basi, kuwapa tu kijitabu ama kuwaambia kuhusu Mungu mwingine, hilo halitafaa kitu, wamishenari wamegundua hilo, hilo halitafaa kitu, hawana budi kuona kitu kinachoonekana ambacho wanaweza kukishikilia.

⁹ Nilikuwa nikizungumza kwenye Kiwanis si muda mrefu uliopita, nikizungumza, na ikawa kwamba mtu aliyeniweka wakfu katika Kanisa la Kibaptisti la Kimishenari alikuwepo. Nilikuwa ndio kwanza nirudi kutoka Afrika, nami nilikuwa ninawaambia, nikasema, nikizungumza juu ya hali za Afrika na jinsi uchumi wao ulivyosawazishwa, na—na kutokuwa na usawa, hasa, na jinsi ambavyo we—wenyeji, na jinsi walivyokuwa wakiendelea, na kuwaambia ya kwamba bila shaka maasi yanakuja, chama cha kikomunisti kinaingia mle na kuyaanzisha, kwa hiyo kutakuwako na maasi.

¹⁰ Na kwa hiyo, na mimi, jinsi nilivyojisikia kulihusu, na kuzungumza juu ya hayo makabila, makabila wenyeji, nami nikamwelezea maskini yule mtu wa msituni, na watu mbalimbali, na jinsi wangekula, chochote tu walichoweza kupata, haidhuru kama kilikuwa na mabuu ndani yake, hayo yalikuwa tu ni nyama za ziada, kwa hiyo hayakuwasumbua.

¹¹ Kwa hiyo basi, na hawa mbu wakining'inia miguuni mwao, hao ni mbu wa malaria, si wa aina hii wanaovuma huku, na kusema, “Wewe ni binamu yangu,” mwajua, na kukuchoma mwiba. Wao si wanafiki, wanapanda tu hapo, na umepata malaria. Lakini hawatawadhuru, wamejenga chanjo kwa miaka mingi.

¹² Nami nikasema, “Vema, kama mmoja akitua juu yetu, tungekufa.” Kama tungaliishi, tungekuwa na malaria kwa angalau miaka kumi na mitano. Na ukipata kumwona mtu yeyote aliye na homa ya malaria, hakika usingeitaka. Anazirai akakosa fahamu siku baada ya siku, na kila kitu, na halafu, ni vigumu sana. Ndipo nikasema, “Basi, katika kula...”

¹³ Na kulikuwa na daktari ameketi pale, naye akasema, “Vema, Kasisi Branham,” akasema, “watu hao si wanadamu, unaona.”

¹⁴ Nikasema, “Loo, samahani, Daktari!” Nikasema, “Hao ni wanadamu tu kama mimi na wewe.” Kabisa. Nikasema, “Jambo

pekee, ni kwamba tumevipata vyote, nasi tukawanyima.” Tena nikasema, “Nipe...”

¹⁵ Kabila la kishamba kabisa kuliko yote Afrika, ni mtu wa msituni, hata wenyewe hawakujua walikuwa wanadamu. Serikali ya Kiingereza iligundua... Mnajua jinsi walivyogundua kwamba walikuwa wanadamu? Walikimbilia mahali padogo namna hiyo, lundo dogo la vichaka, mwajua, nao wakaanza kutetemeka namna hiyo, wala hakuna kitu. Wakaangalia kila mahali, kila kitu kinatoweka tu. Wakaangalia huko kwenye mchanga, vichwa vichache vyeusi vikijongea namna *hii*. Wakajifunika katika mchanga, wakiangalia waone ulianda upande gani.

¹⁶ Na njia pekee waliyojua walikuwa wanadamu, miaka mingi iliyopita, njia ya kwanza waliyojua walikuwa wanadamu, mngetaka kujua jinsi walivyojua? Walikuwa na mbwa. Mbwa hataishi pamoja na chochote ila mwanadamu, hataishi na chochote ila mwanadamu. Na hivyo ndivyo serikali ya Kiingereza ilivyojua ya kwamba walikuwa ni wanadamu.

¹⁷ Sasa, nipe mmoja wa hao wavulana wadogo waliozaliwa, wakati ana umri wa siku mbili tu, ama umri wa miezi sita, hebu nimchukue, mtoto wa mtu wa msituni, hamjui baba yake, mama yake, hamjui yeyote wa kabila lake, hajui chochote ila kuua tu na kula, na wakati akiwa na umri wa miaka kumi na minane, yeye ni mwerevu, amelimika, mwerevu tu awezavyo kuwa. Mnaona? Ana akili, anaweza kufikiria, ana nafsi. Lakini unaweza kushindilia yote utakayo ndani ya mnyama, wala kamwe hutamfanya afikirie, hawezi kufikiria, hana nafsi. Yeye ni mwanadamu.

¹⁸ Ndipo baada ya wao kusema hivyo, kwa namna fulani waliniudhi kidogo, kwa sababu Yesu alikufa apate kumwoko maskini mtu yule wa msituni kama vile alivyokufa apate kuniokoa mimi. Na ni wajibu wangu, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba anapata Injili. Mungu atatuwajibisha kwa jambo hilo, tusipoipeleka kwake. Naam, bwana, Mungu atatuwajibisha. Mnamjua mlinzi ukutani, asipoonya, basi damu inatakiwa mkononi mwake.

¹⁹ Halafu daktari, tulikuwa tukizungumza kidogo, sasa, ndipo mhudumu mmoja akainuka, naye akaanza kusema kuhusu, misheni zake kule. Naye ndiye aliyesema ya kwamba nitageuka kuwa mtakatifu anayejibingirisha.

²⁰ Nami nikasema, “Daktari, unajua, miaka michache iliyopita, uliniambia usiku ule nilipomwona yule Malaika kule juu, uliniuliza kama sikuwa nikila pilipili nyekundu, na kupata jinamizi. Nami nikasema, ‘Kama huo ndio msimamo wa kanisa la Kibaptisti, nitaachilia ushirika wangu nalo sasa hivi,’” mnaona, “nikasema, ‘kwa sababu Mungu aliita, na itakuwa hivyo.’”

"Kasema, 'Ati wewe ukiwa na elimu ya msingi, utaipeleka Injili ng'ambo, wakati maelfu ya wamishenari wana diplomasia?"

"Na—nami nikasema, 'Sijali wana nini, Mungu ananituma mimi.'

"Naye akasema, 'Utafanyaje jambo hilo?"

"Nikasema, 'Hiyo ni juu ya Mungu kufanya hivyo, si mimi, ni juu Yake. Ninawaambia tu ukweli.'"

²¹ Kisha nikasema, "Unakumbuka hilo, bwana?" Nikasema, "Nataka ujue, nilikutana na wamishenari wetu huko, nitawaambia nguvu zake. Hawa hapa wenyeji wanakuja wamebeba sanamu ya matope chini ya mkono wake akiwa na kibandiko juu yake, 'Mkristo.'" Nikasema, "Vipi kuhusu hilo?"

²² Sidney Smith, meya wa Durban, akasema, "Ninaweza kuzungumza lugha ya mtu yule *pale*." Kasema, "Yeye ana kibandiko, yeye ni Mkristo, amebeba sanamu ya matope iliyonyunyiziwa damu ya mnyama," kasema, "hebu tumwulize." Kasema, "Yeye ni Mshangaani, ninaweza kuzungumza Kishangaani." Nikasema... Kasema, "Mwite chochote utakacho."

Nikasema, "Thomas," nilifikiri hilo lingekuwa ni jina zuri, nikasema, "Thomas, je, wewe ni Mkristo?"

"Loo, naam. Naam." Akaongea lugha yake, ikafasiriwa. Yeye ni Mkristo.

Nikasema, "Kwa nini unabeba sanamu hiyo?"

²³ "Loo," akasema, "Kama—kama Amoyah..." *Amoyah* linamaanisha "nguvu zisizoonekana," kama upepo. "Kama Amoyah akishindwa, Mungu asiyeonekana, huyu hatashindwa." Mnaona? Huyu ni Mkristo, mwajua. "Huyu hatashindwa."

Nami—nami nikasema, "Vema, unajuaje hilo?"

²⁴ Akasema, "Vema," baba yake alibeba sanamu ii hii, ndipo siku moja simba akamfukuza, naye akaketi chini, akawasha moto kidogo, halafu akakariri maombi aliyoambiwa na mchawi, yule simba akatoroka.

²⁵ Nami ni—nikasema, "Mimi ni mwindaji wa simba, nami ninajua jambo moja, ya kwamba mnyama yeyote anaogopa moto. Hayo maombi ya mchawi hayakumfukuza, moto ulimfukuza, anaogopa moto."

²⁶ "Loo, vema," Yeye angetafuta usalama kwanza, na kuibeba hiyo, kwa vyovyote vile. Mnaona? Huo ndio Ukristo.

²⁷ Wanaenda huko nje, wamishenari wengi, wanapowaingiza, wanawashusha kwenye mgodi wa almasi, futi elfu moja mia saba chini ya ardhi, wapate kulipa kodi zao. Wanarudi, na inawabidi kucheza dansi mara kwa mara. Mnajua wanapokuwa na dansi, wamishenari wanashuka na kumsambazia vitini mtu ambaye hawezi kutofautisha mkono wa kulia na wa kushoto. Naam.

²⁸ Nikasema, “Tlikuwave? Mnachokiita ulokole, kile mlichokiita mtakatifu anayejibingirisha, niliona elfu thelathini wao wakivunja sanamu zao ardhini na kumpokea Yesu Kristo, wanawake walio uchi walijifunika na mikono yao na kuondoka mahali hapo.” Nikasema, “Hilo ndilo wanalotazamia kuona. Hawajali kuhusu baadhi ya vijitabu vidogo, mungu wao ana nguvu tu kama wale wengine unaozungumzia.” Mnaona?

²⁹ Lakini inapofikia jambo wanaloweza *kuona* ambalo litawashangaza miungu yao, na kuwakomesha wachawi wao, na kuwapooza njiani mwao, na kuona, ndipo wanaamini ya kwamba kuna Mungu anayeweza kutenda kazi. Hiyo ndiyo Injili ambayo makafiri hawana budi kuipata, hivyo tu. Elimu ye—yetu na maadili havitafanikiwa kwa makafiri, hana budi kuona kitu fulani, ha—hana budi kujua ni sahihi.

³⁰ Jambo lile lile huko India, tuliona... Moja ya magazeti lilichapisha makala hiyo hivi majuzi tu wakati ndugu yetu mheshimiwa, Billy Graham, alipopewa changamoto na huyo Mwislamu, naye Billy akashindwa. Sasa, si—simlaumu, ningefanya vivyo hivyo.

³¹ Lakini, kama Mkristo, ningesema, “Hilo haliko katika huduma yangu ya kuhubiri, mimi huhubiri wokovu. Mnaamini ya kwamba Mungu katika Ishmaeli alikuwa ni mwana wa Ibrahimu, ambaye alikuwa, zile baraka. Hebu nizungumze nanyi juu ya yale nijuayo. Ninaweza kuwathibitishia ya kwamba—ya kwamba Isaka, baraka zilikuja kupitia kwa Isaka, wala si kupitia kwa Ishmaeli.” Kama ningalikuwa Daktari wa Ungu kama alivyokuwa, ningalimpa changamoto juu ya hilo.

³² Lakini ningesema, “Sina karama za uponyaji, na kadhalika, lakini tunao ndugu katika dini ya Kikristo, Oral Roberts, na kadhalika, wanaoweza kuletwa jukwaani sasa hivi wanaoweza kuufanya, na ni kweli.” Ningeshikilia beramu yangu ya dini ya Kikristo.

³³ Lakini basi ninii, ga—gazeti lilitoka, nanyi mliona jambo hilo katika *Mbiu Ya Imani*, akasema, “Kwa nini hakuupa huo mkutano changamoto...? Vipi kuhusu huko chini Durban, Afrika Kusini, alasiri hiyo?”

³⁴ Wakati Waislamu walipokuwa wameketi pale na kuona kule kutenda... Wakati mwanamke yule wa Kiislamu alipokuja jukwaani, Roho Mtakatifu akamwambia, kasema, “Wewe ni Mwislamu, kwa nini ukaja kwangu?”

Akasema, “Nilifikiri ungeweza kunisaidia.”

Nami nikasema, “Je, uliwahi kusoma Biblia kuhusu yale Yesu aliyofanya, jinsi alivyojua siri za moyo wao?”

“Ndiyo.”

Nikasema, “Unaonaje kuhusu hilo?”

“Vema,” akasema, “Ninaamini ya kwamba Yesu alipanda farasi akaingia Utukufuni, akakimbia kuingia Utukufuni. Alikuwa ni nabii.”

Nikasema, “La, Yeye alisulubiwa, akafa, na kufufuka tena, na Roho Yake inaishi hapa leo hii.”

“Sijui kuhusu hilo.”

³⁵ Nikasema, “Vipi kama Yeye akirudi na kufanya jambo lile lile alilofanya wakati huo? Je, hilo lingekuthibitishia kama Yeye atatenda papa hapa kupitia kwetu jinsi alivyotenda alipokuwa hapa duniani?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Je, umewahi kusoma Agano Jipya?”

“Mara nyingi.”

³⁶ Nami nikasema, “Vema basi, kama Yeye atanifunulia wewe ni nani, kile ulicho, na kile kilichokuleta hapa, kile umekuwa, na kile kitakachokupata, utakubali?”

Akasema, “Ndiyo.”

³⁷ Maelfu ya Waislamu wakiketi huko nje. Nami nikasema, “Ni wangapi wenu ninyi Waislamu watalikubali?” Wakati mkalimani alipolisema, mikono ikainuliwa.

³⁸ Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kutenda kazi na kumwambia yeye alikuwa ni nani, alitoka wapi, alimwendea daktari yupi, jina lake lilikuwa nani, tukalizungumzia namna hiyo, na kusema alikuwa na uvimbe kwenye ovari yake, na akaponywa wakati huo. Utukufu wa Mungu ukashuka, nao Waislamu elfu kumi wakamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi.

³⁹ Na ndiyo, alasiri hiyo sijui ni wangapi zaidi waliokuja, walikadiria pale elfu kumi. Na wakati, alasiri hiyo, wakati mvulana huyo hata hana akili timamu, akiongozwa na mnyororo shingoni mwake, wakati Roho Mtakatifu alipomwambia jinsi alivyozaliwa, naye alizaliwa hivyo, akamwambia mama na baba yake, waliokuwa wameketi nje kwenye kusanyiko, yapata watu mia moja na hamsini elfu, mia mbili, na kusema, “Ndugu yako, unayemwazia, yuko huko nje kwenye kusanyiko, alikuwa amempanda ama mbuzi mweupe, au mweupe, ama, mbuzi wa manjano, ama mbwa, akaumia magoti yake, anatembea kwa marungu mawili, lakini BWANA ASEMA HIVI, ameponywa.”

⁴⁰ Na yapata jengo moja la mji kupitia kwenye huo uwanja wa maonyesho, huyu hapa anakuja amebeba marungu yake, akipiga mayowe, akiruka juu chini kwa nguvu alivyoweza, ameponywa. Ilituchukua kama nusu saa kuwatuliza.

⁴¹ Ndipo nilipoangalia nyuma, nami nikamwona mtu huyo katika ono amesimama pale kwa miguu yake, mzima kadiri alivyoweza kuwa, alitembea kwa mikono na miguu yake namna

hiyo, hata hana akili timamu, nilipozungumza naye, alitaka kunichezea da—dansi, dansi ya kikabila, ndipo nikaangalia, nami nikamwona amesimama pale, nikajua hilo lilikuwa ndilo. Unapona ono hilo, halitashindwa.

⁴² Ndipo nikaliangalia hilo kusanyiko, nikasema, “Ni wangapi hapa ndani. . . ? Huyu hapa mtu hapa, maskini, mtu aliyelemaa, angalia ni hali gani aliyomo.”

Kulikuwa na daktari Mwingereza pale, juu ya maskini mvulana huyo mwenye mkengeza, alisema, “Bw. Branham, ulimfanyia nini mtoto huyo?”

Nikasema, “Kamwe sikufanya lolote.” Nikasema, “Hata sikumwomba. Walimwinua tu jukwaani.”

⁴³ Kasema, “Mimi nilimweka jukwaani.” Kasema, “Alikuwa na mkengeza alipopitia *hapa*, akatokea *pale* bila mkengeza.” Kasema, “Kwani umemfanyia. . . Je, ulimfanyia hiponozi mtoto huyo mchanga?”

⁴⁴ Nikasema, “Daktari, hivi Shirika la Tiba la Kiingereza lilikupa leseni ya kufanya kazi ya udaktari? Vipi kuhusu ninyi Waingereza mnaofanya hiponozi *hiyo* yote?” Nikasema, “Kwa nini msianyoshe macho yake?” Nikasema, “Ikiwa hiponozi itanyosha macho, ninyi jamaa afadhali mwanze kufanya hiponozi.” Nikasema, “Ulijua alikuwa na mkengeza *pale*.”

Ndipo Ndugu Baxter akaja naye alikuwa akimwondosha. Ndipo nikasema, “Achana naye. Acha azungumze.”

Naye akasema, “Utasababisha tu ghasia huko nje sasa, unachukua muda na mtu huyo.”

Nami nikasema, “Vema, hebu kidogo.”

Akasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani.” Kasema, “Ninaamini kuna Mungu, Yeye yuko katika hayo mayungiyungi.”

⁴⁵ Na, loo, laiti ninyi wanawake mngaliyaona hayo mayungiyungi. Mayungiyungi ya kalla yana upana wa inchi kumi na nane, namna *hiyo*, mazuri ya manjano na meupe, ya mwitu, yakikulia moja kwa moja msituni. Nalo jukwaa lilikuwa limejaa hayo. Nikasema. . .

Akasema, “Kuna Mungu, namna fulani ya uhai katika yungiyungi hilo, lakini je, Yeye ni dhahiri vya kutosha kuyafanya hayo macho ya mvulana mwenye mkengeza yanyoke?”

Nikasema, “Ulimchukua kutoka jukwaani, ukamwondoa hapa.”

Akasema, “Je, huyo Mungu yupo?”

Nikasema, “Naam, bwana, Yeye yupo hapa sasa.”

⁴⁶ Akaenda moja kwa moja kwenye maikrofoni, mikrofoni kubwa mno, inayoning’inia namna *hiyo*, kwa sababu ilitubidi kuzungumzia majengo mawili au matatu ya mji kila upande na

kurudi nyuma *hivyo* jengo moja la mji au zaidi, maelfu ya watu mara maelfu, akasema, “Sasa ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi.”

⁴⁷ Wakati, nilipokutana naye huko Durb-...Johannesburg tulipokuwa tunaondoka. Nilimsikia mtu fulani akipaza sauti, “Ndugu Branham!” Hiyo, mwajua, hiyo lafudhi ya Kiingereza cha kikukni waliyo nayo; akakimbia huko nje kwenye—kwenye daraja wakati walipokuwa wamechora mistari, huku wote, polisi walipanga mistari juu chini namna *hii*, kusudi watu wasiweze kuingia mle. Walinileta kwenye motokaa na kuniondosha, nami nikafika huko nje, naye akasema, “Ndugu Branham!” Akapenya akakimbia huko nje, akanikumbatia, akaanza kunena kwa lugha, alikuwa ameiwa kwenye huduma ya umishenari. Loo, jinsi nilivyopenda kumwambia Dk. Davis na hao wengine hayo!

⁴⁸ Nikasema, “Kile mnachokiita ulokole kilileta watu wengi zaidi kwa Kristo katika mkutano mmoja kuliko makumi ya maelfu, mara mamilioni ya dola tulizoweka kwa wamishenari kwa miaka hamsini iliyopita huko Afrika.”

⁴⁹ Hiyo ni kweli. Jambo ndilo hilo. Hebu na tulifanye lilete faida, ndugu. Dola hizi ni mali ya Mungu, na hebu tuzifanye zikauletee faida Ufalme wa Mungu, kwa watu ambao kweli wanazihitaji.

⁵⁰ Mvulana huyo, aliposimama, nilimwambia, nikasema, “Simama, Yesu Kristo amekuponya.”

⁵¹ Hakujuua nilichokuwa nikizungumzia. Naye mkalimani akamwambia, bado alitaka kucheza dansi. Nikaushika huo mnyororo na kumwinua namna *hii*, alikuwa na ukosi shingoni mwake kama mnyama. Na wakati aliposimama, alikuwa kabisa...Mara ya kwanza maishani mwake kusimama kwa miguu yake. Machozi makubwa yalitiririka kwenye tumbo lake jeusi namna hiyo, na hapo akasimama, mwenye akili timamu, amesimama kwa miguu yake.

⁵² Maelfu mara maelfu wakaanguka chini. Nao walikadiria—walikadiria miujiza elfu ishirini na tano ya ajabu sana ilitukia papo hapo. Hapakusalia wengine wa kuombewa, walitoka kwenye vitanda vya wagonjwa, machela, viti vya magurudumu, kila kitu kingine. Na kesho yake asubuhi, kulikuwa na malori saba makubwa ya mizigo, haya malori makubwa mno, marefu ya Kiafrika, yamejaa mikongojo na viti vya magurudumu, nao walikuwa wakishuka kuja barabarani.

⁵³ Sidney Smith, meya wa Durban, alikuja dirishani, kasema, “Angalia nje mtaani.”

⁵⁴ Hawa hapa, wamekuwa katika vita vya kikabila, wakiwa na amani wao kwa wao, wakitembea mitaani, wakiimba, “Mambo yote yanawezekana, amini tu.” Loo! Hmm!

55 Hatuwezi kuwa na mkutano wa namna hiyo Marekani, tunajua mengi kupita kiasi, tunajua mengi kuyahusu, mnaona, sisi ni werevu kupita kiasi kwa hilo, mnaona. Endeleeni, tunazikosa tu baraka, hivyo tu, mnaona. Sisi... Sasa, ninyi watu mnaweza kuwa nalo, hakika, mnaweza kuliona likitukia hapa, lakini ninamaanisha taifa, kama hilo lilivyo huko. Mungu awabariki.

56 Ndugu Kopp, uko hapa usiku wa leo? Mimi... Ndugu Kopp, Ndugu Leroy Kopp, amekuwa hapa mikutanoni. Nilitaka kumpongeza kwa ile makala aliyoandika, *Wayahudi Hutafuta Ishara*, alikuwa akizungumza kuhusu huduma yangu mle ndani. Na kama uko hapa, Ndugu Kopp, na unaisikiliza sauti yangu, mimi, hakika, ninakuja Israeli. Hilo ndilo...

57 Wayahudi wanataka kuona ishara ya nabii, wanaamini Masihi atakuwa ni nabii, wangali wanaiamini.

58 Ni wangapi wamesikia habari za Lewi Pethrus? Hakika, mlizisikia, kiongozi wa kanisa la Stockholm, Kanisa la Filadelfia, huduma ya Kipentekoste iliyo kubwa kuliko zote ulimwenguni. Basi alituma Agano Jipya milioni moja kule chini.

59 Ni wangapi waliwahi kuona gazeti la *Look* na *Life*, yakionyesha hizo ndege zikiingia, zikiwabeba hao Wayahudi kutoka huko chini Irani, wote huko chini, yapata tu miaka miwili au mitatu iliyopita? Hapo ndipo walipopata ile makala, *Dakika Tatu Kabla Ya Usiku Wa Manane*.

60 Sasa, walipowapa hizo Agano, wao husoma kuanzia nyuma kwenda mbele, nanyi mnajua jinsi Kiyidi kinavyoandikwa, basi wakasema, "Iwapo Huyu ndiye Masihi, Yeye aliahidi jambo hili, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii. Masihi atakuwa ni nabii, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii nasi tutampokea."

61 Loo, jamani, hilo liliuchochea moyo wangu! Moja kwa moja mahali pale pale ambapo Roho Mtakatifu alishuka kwa mara ya kwanza.

62 Mnaona, hamwezi kuwa na wasomi. Hamumkatikati Mungu katika vipande vinne ama vitano na kumpa Myahudi, hana budi kujua ya kwamba ana Mungu. Kwa hiyo basi... Kwa hiyo yeye... Ma—mambo ya kiakili hayatafanya kazi kwake. La, bwana, hana budi kujua jambo hilo.

63 Na kwa hiyo basi, nikawaza, "Hilo si litakuwa zuri sana kama ningewakusanya karibu mia tano wao pamoja huko nje, na kusema, 'Tokeni mwende miongoni mwenu, mkawaletе watu hapa juu, mwone kama Masihi angali ndiye Nabii,' na moja kwa moja kwenye uwanja uo huo ambapo wanamkubali Yeye kama Mwokozi, halafu uwaombe wainue mikono yao na kumpokea Roho Mtakatifu"?

64 Ni wakati wa jinsi gani! Mnajua nini? Hiyo itamaliza kipindi cha wakati wa Mataifa, Injili itawaendea Wayahudi,

watawafanyia watu wao—wao umishenari kwayo. Israeli ni taifa, sisi sote ni mataifa, bali Israeli ni taifa, nao Ufalme utawarudia Israeli, siku moja, kama Isaka alivyomwambia Yusufu, “Ule mzabibu utarudi utande ukutani, siku moja.” Hiyo ni kweli.

⁶⁵ Sasa, asanteni sana, kila mmoja wenu, kwa wema wenu, ushirikiano wenu wote mzuri. Ninataka kulishukuru Tawi la Wafanyabiashara wa Full Gospel, kwa kuwa ninaamini hii ni mara tatu, mbili ama tatu mfululizo walinidhamini kuwa hapa, ushirikiano mzuri wa ninyi wahudumu. Mungu daima awe pamoja nanyi nyote. Tawi hili na likue, makanisa yenu na yakue, Bwana na apate utukufu kutoka kwa yote yanayofanywa au kusemwa.

⁶⁶ Sina budi kuondoka mapema asubuhi sasa kwenda Tacoma, halafu kutoka huko kwenda Yakima. Nami ninangojea wakati wa kwenda ng’ambo, upesi tu niwezavyo, kufanya ziara ya ulimwengu miongoni mwa watu waliofukuzwa wa Ulaya, na Asia, na Mashariki, na—na Mashariki ya Mbali, na kadhalika, kuhubiri Injili.

⁶⁷ Kama ikitokea nisirudi tena, nitakutana nanyi ng’ambo ya mpaka kule. Kama mkiondoka, nami nirudi tena kuwaona, natumaini nitawaona, lakini kama mkiondoka kabla sijarudi basi, bado nataka kuwaambia: Nitakutana nanyi ng’ambo ya mpaka nikiwa na ushuhuda ule ule nilio nao sasa: Yesu huokoa na kuponya, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mungu awabariki daima.

⁶⁸ Kama ninaweza kuwa faida kwenu, msaada, nitumieni kadi, barua, chochote kile. Ikiwa wewe. . . Hivi hapa vitambaa vya maombi vimewekwa hapa, kama huna kimoja hapa usiku wa leo, unataka kimoja, niandikie tu: Sanduku la Posta 325, Jeffersonville, Indiana. Weka kimoja katika Biblia yako kwenye Matendo 19, wakati wa dharura, kiweke juu ya mgonjwa wako na anayeteseka.

⁶⁹ Hakuna malipo kwake, hata kidogo, wakati mwingine watu hunitumia pesa kidogo kunisaidia kulipia stempu, ninalipa mamia ya dola kwa juma kwa ajili ya stempu. Lakini wao, wakati mwingine wao. . . Si lazima ufanye hivyo, hiyo haihitajiki, lakini kama ukifanya hivyo, hivyo ndivyo wanavyozitumia.

⁷⁰ Na yote yanaendeshwa kupitia maskanini, hakuna kitu kinachonijia, yote ni kupitia kwa Maskani ya Branham, hivyo ndivyo imekuwa sikuzote. Sikuzote nimewashuhudia, nikirudia mara nyingi, ya kwamba ujira wote kutoka kwa ninii, mimi hupata mshahara, na michango yote kutoka kwenye mikutano hupelekwa maskanini, nayo inatumiwa kwa misheni za kigeni, hiyo ni kweli, kusaidia kueneza Injili, si kwa kitu kingine chochote ila kueneza Injili, hivyo tu. Na Bwana awabariki.

⁷¹ Sasa ninataka kuwaomba fadhili kabla sijaanza kuwahubiria kwa muda kidogo tu. Niliahidi kumwomba kila

mtu aliye na ka—kadi, nami nafikiri tuna kadhaa hapa. Billy aligawa lundo zima kamili la hizo muda mfupi uliopita, alisema, kwa hiyo ninataka kuwapitisha mstarini na kuwaombea. Na sasa tunataka kupata kitu fulani kidogo kujenga imani kidogo. Ni wangapi wenu watakaoniombea, mtu anayeyahitaji kweli? Asanteni. Ninapoenda, niko tu katika mabadiliko sasa kati ya huduma moja na nyingine, na daima huanzisha kitu fulani kidogo. Na sasa ni—nina—ninamngojea Bwana. Nanyi mwe na hakika kwamba mnaniombea, kweli nayahitaji.

⁷² Ndugu Rose, je, ulitoa ushuhuda wako hapa kuhusu jinsi Mungu amekuponya, na kadhalika? Ulipaswa kufanya hivyo. Na ni ushuhuda mkuu. Tunampenda ndugu huyu. Yeye ni... Mke wangu anamwogopa sana, mtu pekee aliyewahi kumleta jukwaani. Alikuwa ameketi pale chini, kidogo ana soni, mwoga, hata hataki niseme yuko mkutanoni, mwajua. Halafu basi, mwenye haya sana, basi Ndugu Rose alisema, “Tunaye Dada Branham hapa usiku wa leo. Njoo moja kwa moja jukwaani.”

Akasema, “Ninamwogopa sana mtu huyo.”

⁷³ Kama kuna sifa yoyote ya kuiendea familia ya Branham, acha imwendee yeye, yeye ndiye anayezistahili, mke wangu, mmoja wa wanawake Wakristo wazuri sana ninaowajua ulimwenguni. Yeye ni miongoni mwa Wateule, nina hakika. Mungu daima aibariki nafsi yake shujaa, thawabu yake ni kubwa Ng’ambo ya pili.

⁷⁴ Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi kwa maombi. Ni wangapi wanataka kukumbukwa usiku wa leo, mnapoinua mikono yenu?

⁷⁵ Baba yetu wa Mbinguni, tunachukua muda. Hatujui kitakachotukia kati ya sasa na wakati mwingine tutakapokutana, huenda tukawa ng’ambo ya mto katika ile Nchi nyingine. Kama hiyo ndiyo kura yetu, Bwana, basi na tuwepo kwenye siku hiyo. Ninakuomba Wewe, Mungu mwingi wa rehema, ya kwamba hakutakuwako na mtu mmoja atakayekosekana kwenye siku hiyo, jalia kila mtu awepo, kila mtu aliye hapa usiku wa leo, kila mwenye dhambi apate kuokolewa, kila mtakatifu anaweza kuendelea mbele, akishikilia mpaka mwisho utakapokuja. Jalia aliyerudi nyuma arudi katika ushirika tena, hebu ajue ya kwamba hajapotea, ameteleza tu kwa dhambi zake, nao uteute wa maneno ya ibilisi umemfanya ateleze aondoke kwenye barabara kuu. Mungu yuko tayari usiku wa leo kumrudisha.

⁷⁶ Leta Moto kanisani, Bwana, Moto wa Roho Mtakatifu. Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Wabariki wale walio wahitaji, kila mkono ulioinuliwa. Mwenyezi Mungu, unajua kila haja waliyo nayo; wao ni wa thamani moyoni mwangu. Na kama ni wa thamani moyoni mwangu, ni wa thamani zaidi jinsi gani kwa moyo Wako? Kwa kuwa Wewe ulitoa maisha Yako kwa

ajili yao. Na kama malipo, Bwana, Wewe ulinitia mafuta, na kunituma nje nikawahubirie habari njema za Ujumbe huu mzuri wa Bwana Yesu, kwa kuonyesha ishara na maaajabu ya kufufuka Kwake na kuonekana Kwake hivi karibuni. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba.

⁷⁷ Nasi tunaomba ya kwamba, usiku wa leo, ibada itakapokwisha, hakutakuwako na mgonjwa mmoja wala mnyonge miongoni mwetu. Tuna furaha sana usiku wa leo, Bwana, ambapo viti vya magurudumu vingi, vinne ama vitano, vilikuwa hapa mwanzoni, hatuvioni usiku wa leo, tunajua ya kwamba baadhi yao wanatembea huku na huku, baadhi yao wanashuhudia uponyaji wao. Watu kwenye mikongojo, wale walio wagonjwa na wanaoteseka, ugonjwa wa tumbo, ugonjwa wa moyo, sasa wanafurahia afya njema, hilo linamaanisha mengi kwangu, Bwana, sana kwao, kujua ya kwamba tunaona ishara za Mfalme kambini. Tujalie, Bwana, kwamba Yeye daima atabaki pamoja nasi. Nasi tutampenda na kumtumikia, mpaka tutakapomwona uso kwa uso.

⁷⁸ Bariiki Maneno tunayosoma sasa, na jalia yawe Taa, Nuru kwa njia yetu kutuongoza karibu na Yeye. Tunaomba, katika Jina Lake la thamani. Amina.

⁷⁹ Hebu na tufungue usiku wa leo Maandiko mawili ambayo nimeyachagua kwa ajili ya ibada ya kumalizia, na moja la hayo ni Luka mlango wa kwanza, na lingine ni Mathayo 24:35. Hebu na tusome, tuanze kusoma Luka katika mlango wa kwanza wa Luka, kuanzia kifungu cha 26. Sasa sikilizeni kwa makini tunaposoma:

Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti,

Kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo lilikuwa Mariamu.

...malaika akaingia nyumbani kwake, akasema, Salamu, wewe...umepewa neema sana, Bwana yu pamoja nawe, umebarikiwa miongoni mwa wanawake.

Naye alipomwona alifadhaika kwa sababu ya maneno yake, akawaza moyoni mwake...akilini mwake, salamu hii ni ya namna gani.

Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. (Mungu asifiwe!)

Na tazama, utachukua mimba, na kuzaa mtoto mwanamume, na jina lake utamwita YESU.

Na Yeye atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu: na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake:

Naye atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele; na ufalme wake utakuwa hauna mwisho.

Mariamu akamwambia malaika, Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?

...malaika akajibu, akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli: kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitakatifu kitaitwa Mwana wa Mungu.

Na, tazama, binamu yako Elisabeti naye amechukua mimba ya mtoto mwanamume katika uzee wake: na mwezi huu ni mwezi wa sita kwake, aliyelitwa tasa.

Kwa kuwa hakuna neno lisilowezezekana kwa Mungu.

...Mariamu akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu sawasawa na neno lako. Kisha malaika akaondoka akaenda zake.

80 Mathayo 24:35:

Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

81 Sasa nataka kuzungumza usiku wa leo, Bwana akipenda, juu ya *Neno La Mungu Lisilobadilika*.

82 Sijui kama Miner Arganbright yuko humu jengoni, Ndugu Arganbright. Nimemwona kwenye mikutano kadhaa, nami nilikuwa na ujumbe kwa ajili yake. Lakini na—naamini... Loo, naam, ninataka kuwa na hakika ya kukuona, Ndugu Arganbright. Ninataka kukutana nawe tarehe 20 Oktoba. Anaelewa lugha hiyo. Sababu ya kumwita mtu huyu *Miner*, sijui, sitakubaliana na baba na mama yake, isipokuwa tu iwe ni katika kimo chake, kwa sababu, ana moyo kama wa jitu.

83 Ni wangapi wanaomjua Ndugu Arganbright? Sisemi jambo hili mbele zake, ningelilisema asingekuwa hapa, ndugu mzuri na maskini mke wake mzuri, Mwairishi. Nimekuwa nyumbani kwao, nimekuwa pamoja naye gizani na mahali mbalimbali, mume na mke Wakristo wenye nguvu, wazuri, wanaopendeza. Ninaamini ya kwamba mke wake ametoka karibu na mahali fulani hapa, alikuwa mkutanoni, pia, sijui kama yuko hapa usiku wa leo au la. Kila mtu anayemjua, yeye ni mpenzi kwa wote, kwa mkwewe, ama watoto, majirani wote, kila kitu kwenye kile tunachokiita Kilima cha Sayuni kule chini, yeye ndiye mpenzi wa ubavu huo wa kilima. Kwa hiyo, tuna furaha kwamba Ndugu Arganbright amehesabiwa miongoni mwa wale waliokombolewa, na Dada yetu Arganbright. Bwana na awabariki sana.

84 Sasa, ilikuwa karibu mapambazuko, nadhani ilikuwa a—asubuhi njema, hapana shaka ilikuwa mnamo wakati huu wa mwaka, yapata Julai. Huyu Mtoto mchanga alizaliwa Aprili. Najua mapokeo yanasema Desemba, lakini hilo kabisa

haliwezekani, hiyo ni kanuni ya imani. Asingeweza kuzaliwa Desemba huku wachungaji wakiwa kando ya vilima, futi sita ama nane za theluji kule wakati huo. Kwa hiyo, Yeye alizaliwa Aprili wakati maisha yote mabichi kwa kawaida huchipuka, wakati huo.

⁸⁵ Alikuwa anaenda zake kisimani, na huku maskini huyo mjakazi akitembea barabarani akiwa na ule—ule mtungi wenye mikono miwili chini ya mkono wake, alikuwa anaenda kuchota maji ya asubuhi. Na hapana shaka ilikuwa ni mapema sana, na ilikuwa Jumatatu, nadhani. Na labda ilimbidi kufanya ziara kadhaa, kwa sababu, kwa kawaida, Jumatatu ni siku ya kufua. Hiyo ni kweli, akina dada? Hivyo ndivyo ilivyo nyumbani kwetu, na kila siku, kwa hiyo, ukiwa na kundi la watoto.

⁸⁶ Lakini kwa kawaida wanaiita Jumatatu ya Bluu kwa sababu ya wanawake kufua nguo Jumatatu. Nilikuwa nikiiita Jumatatu ya Bluu, kwa sababu ilinibidi kubeba maji kwa karibu nusu maili kutoka kwenye chemchemi, kuyamimina kwenye maskini birika kubwa la kale huko nje, kisha kukata kuni na kuzitandaza chini yake. Loo, jamani, nina furaha wana mabomba siku hizi.

⁸⁷ Halafu basi, alipokuwa akishuka kwenda barabarani, alikuwa akiwazia juu ya siku iliyotangulia, juu ya ma—mazungumzo yaliyokuwa yamezungumziwa na yeye na mumewe aliyemposa, ama mume wake mchumba, walipokuwa wameketi barazani, kama ilivyokuwa desturi yao, baada ya ibada za asubuhi, walipokuwa wakienda kanisani kule Nazareti. Nao wakatoka, wakaketi barazani baada ya mlo wa adhuhuri.

⁸⁸ Naye Yusufu, atakayekuwa mumewe, alikuwa seremala, naye alijenga majengo mazuri. Lakini sasa, alikuwa akijenga moja ambalo lilipaswa kuwa na uangalizi maalum kwa hili, kwa sababu alikuwa akimpeleka maskini bibi-arusi wake mrembo kwenye hili.

⁸⁹ Nasi tutasema kwamba kutoka kwenye baraza, baraza ya mbele, mahali walipokuwa wameketi, labda ilikuwa imeelekea kusini, nalo jua lingezunguka upande ule mwingine, nao utukufu wa asubuhi karibu na maskini baraza hiyo ulifanya kivuli. Nao wangepaswa kuangalia upande wa pili wa bonde, na juu kando ya kilima ambapo nyumba hii ndogo ilikuwa ikijengwa. Nayo milango yote ilibidi iwe na mguso fulani tu ambapo Mariamu hangelizimika kuisukuma kwa nguvu, angeweza tu kuusukuma, nao ungefungika kwa urahisi. Yusufu alitaka kuhakikisha hili, hauna budi kuwa na mguso mdogo, maalum.

⁹⁰ Basi kila Jumapili desturi yao ingekuwa, kuketi huko nje na kuangalia ng'ambo ya bonde, na kuzungumzia jinsi hilo lango dogo halina budi kuwa na umbo la moyo ndani yake, kwa sababu walipendana, na ile meza ndogo, jinsi inavyopaswa kutengenezwa, na fenicha zao zilikuwa zingizwe ndani ya nyumba.

⁹¹ Basi walipokuwa wameketi pale siku hii baada ya mlo kwisha, naye Ana, mamake Mariamu aliyekuwa mjane, kasema, “Watoto, nendeni nje barazani, nami nitaosha vyombo leo.”

⁹² Basi alipokuwa akiosha vyombo, huku Yusufu ameketi kitako akijivunia huo upishi, bila shaka, na—nao walikuwa wakiangalia upande wa pili, walikuwa wakizungumzia mahubiri waliyosikia asubuhi hiyo.

⁹³ “Loo,” Mariamu akasema, “Yusufu, hivi haikuufurahisha moyo wako wakati rabi aliponena juu ya Mungu mkuu Ambaye yuko juu ya watu wetu? Hivi haikukusisimua wakati rabi alipochukua somo lake kutoka katika Mwanzo, ama, Kutoka yapata mlango wa 13, ambapo alisema kwamba Nguzo ya Moto ya Malaika wa Mungu ingewatangulia? Na jinsi ambavyo Mungu alikutana na Musa, yule nabii mkuu, katika Nguzo ile ya Moto, na kusema naye upande wa nyuma ya jangwa, naye Yehova aliwajali sana watu Wake wa kale, Israeli, hata asingeweza kuwasahau, na jinsi alivyosema, ‘Nimeona taabu zao na huzuni zao. Ninalikumbuka Neno Langu, nami nimeshuka kuwakomboa.’

“Loo,” akasema, “Yusufu, hivi hilo halikuuchangamsha moyo wako wakati ra—rabi aliposema, ‘Mungu alisema, “Ninakumbuka Neno Langu, ahadi Yangu”’?”

⁹⁴ “Loo, naam, Mariamu, iliuchangamsha moyo wangu. Na jinsi alivyoshuka kwenda kule Misri, nabii huyu mkuu, akaonyesha ishara kuu na maajabu, akawaleta kwenye Bahari ya Shamu, naye Yehova ndiyo kwanza aifungue Bahari ya Shamu. Walipokuwa na njaa, Mungu aliwapulizia kware na kuwalisha. Walipoona kiu, walinena na Mwamba, wakupata maji kutoka Humo. Na yote waliyohitaji, Yehova alihakikisha ya kwamba yalishughulikiwa. Waliposhikwa na ugonjwa, na kuumwa na nyoka, na kufanya dhambi, Yehova alimwagiza Musa kufanya nyoka wa shaba na kumweka juu ya mlingoti.”

“Ufasiri wako wa hayo ni nini Yusufu, mpenzi wangu?”

⁹⁵ “Vema, Mariamu, ninaamini ya kwamba hilo lilimaanisha kwamba kungekuwako na sadaka ya dhambi siku moja. Kwamba huyo nyoka wa shaba, ile shaba ilimaanisha hivyo, huyo nyoka mwenyewe alikuwa ni dhambi iliyohukumiwa tayari, na shaba hiyo ilikuwa ni hukumu ya Kiungu, na hukumu ya Kiungu ingekuwa juu ya Mtu mmoja siku moja, na ingekuwa upatanisho kwa ajili ya uponyaji milele. Nyoka hiyo ya shaba ilimaanisha hivyo, naamini.”

⁹⁶ Basi walipokuwa wameketi pale na kuzungumza, lakini yeye akasema, mara moja, “Lakini mliona, aliharibu mahubiri yake? Papo hapo mwishoni mwa mahubiri yake, alisema, baada ya kusimulia jinsi Yehova alivyokuwa mkuu, ‘Sasa, siku hizo zote zimepita, Yehova hafanyi miujiza tena. Hakuna kitu kama Mungu kuwaponya wagonjwa, ama kufanya chochote namna

hiyo. Yehova anatutarajia tu kuwa Mafarisayo wazuri, na kwenda kanisani, na kulipa zaka zetu na matoleo yetu kanisani, na kumjengea mahali pazuri, na kwenda huko na kuimba nyimbo kila asubuhi ya Sabato na kumwabudu. Hilo ndilo Yehova analotarajia siku hizi.’

⁹⁷ “Unajua, Yusufu, ni vigumu kwangu kukubaliana na huyo rabi mzuri juu ya hilo. Ninaamini kama Yeye aliwahi kuwa Yehova, Yeye angali ni Yehova; kama Yeye aliwahi kuwa mwenyezi, Yeye angali ni mwenyezi.”

⁹⁸ Mwajua, Mungu daima ana masalia ya watu watakaomwamini, mahali fulani. Sikuzote ana masalia, mtu anayeweza kuweka mikono Yake juu yake, anao sikuzote na atakuwa nao daima.

⁹⁹ Ndipo, alipokuwa akisafiri mbele kidogo, alikumbuka pia, wakiwa wameketi pale ba—barazani na walikuwa wanazungumza, ilikuwa ni kawaida yao kusoma Maandiko Jumapili alasiri, kwa hiyo anarudi ndani ya jengo, na kutoa kile kikapu kidogo, na kuleta Magombo.

¹⁰⁰ Siku hizo haikuwa katika kitabu kama *hiki*, ilikuwa ni gombo, sura moja ya Isaya, na Yermia, na vyote vimewekwa kwenye ngozi katika gombo, na kufingirishwa, na kuwekwa ndani ya kikapu. Hawakuwa na karatasi siku hizo, kwa hiyo waliyaweka kwenye ngozi iliyokuwa imetengenezwa.

¹⁰¹ Kwa hiyo, akasema, “Yusufu, wewe chagua Gombo la kusoma alasiri ya leo, Jumapili hii alasiri.”

Naye akasema, “Loo, Mariamu, nyosha mkono ulichukue, mpenzi.”

Ndipo akainyosha maskini mikono yake mirembo, huku macho yake yakiangaza, akalichukua lile Gombo na kumkabidhi.

Akasema, “Unajua, Mariamu, ningetaka kukusikia ukisoma.”

¹⁰² Naye alikuwa na Isaya, basi akasoma katika Isaya, na kuanza kusoma mpaka akafikia Isaya 9:6:

...kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume: na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake: naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, . . . Mungu mwenye nguvu, . . . Mfalme wa Amani.

¹⁰³ Ndipo akasimama, akasema, “Yusufu, umefunzwa vizuri katika Maandiko, nabii alikuwa akinena juu ya nini aliposema hivi: ‘Kwa ajili yetu amezaliwa mtoto Mwanamume?’”

“Vema,” Yusufu akasema, “Mariamu, ninaamini alikuwa akimaanisha Masihi, yule Masihi ajaye ambaye Musa alinena habari zake.”

“Vema,” akasema, “Yusufu, Masihi angekuwaje? Je, atakuwa Mungu mwingine? Au Yeye atakuwa . . . ? Atakuwa na uhusiano gani na Mungu?”

Yusufu akasema, “Yeye atakuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Mungu atadhihirishwa katika Mwana huyu ambaye atamwumba.”

“Vema atamwumbaje huyu Mwana?”

¹⁰⁴ “Loo, Mariamu mpenzi wangu,” hapana shaka Yusufu alisema, “Unajua, Isaya pia alisema katika 7:14 pale, ya kwamba ‘Bikira atachukua mimba, naye atazaa Mwana, Naye atakuwa Imanueli, Mungu pamoja nasi.’”

¹⁰⁵ Loo, macho yake marembo hapana shaka yaliangaza. Basi wakati jioni ilipokaribia kuingia giza, walijiandaa kwenda kanisani kusikia ujumbe mwingine kutoka kwa rabi, basi hilo Gombo likaondolewa.

¹⁰⁶ Basi alipokuwa akitembea asubuhi hiyo, alikuwa akiwazia juu ya mambo hayo, ndipo akapiga kona. Basi alipopiga kona, ninaamini lazima Nuru ilimulika, naye akaangalia juu, nalo jua zuri la Galilaya lilikuwa linachomoza. Kulikuwako . . . Hapana shaka alidhani ilikuwa ni mmemeteko kutoka kwenye mwamba, ama kipande cha chuma, kilichosuguliwa vizuri; hawakuwa na glasi siku hizo, sidhani. Kwa hiyo wao . . . Hapana shaka waliwazia jambo fulani, lakini Nuru ilionekana kumulika mbele yake, akaangalia kote, hakuona chochote, naye akaanza kwenda.

¹⁰⁷ Mwajua, ni wakati tunapomwazia, hapo ndipo Yeye anapotukaribia. “Nikaribieni, nami nitawakaribia,” asema Bwana. Laiti tungaliweza kuweka mawazo yetu mbali na mambo ya ulimwengu, na upumbavu mwingi sana ambao hatuna shughuli kuuwazia! “Mawazo ya moyo wangu na yakubalike Kwako, Ee Bwana.”

¹⁰⁸ Ilikuwa kwenye Pasaka ya kwanza wakati wale mitume wawili, Kleopa na rafiki yake, walipokuwa wakienda zao Emau, walipokuwa wakizungumza habari Zake, ambapo Yeye alitoka kwenye kile kichaka na kuanza kuzungumza nao. Ndipo basi akajitambulisha kwao kwa kufanya mwujiza, kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Nao wakakimbia upesi wakarudi, na kusema, “Hakika, Bwana amefufuka, na ametutokea.”

¹⁰⁹ Sasa, Mariamu alikuwa akimwazia, na alipokuwa akiendelea, kwa ghafla, akainua kichwa chake tena, alikuwa na hakika wakati huo. Papo hapo mbele zake, ilisimama Nuru kuu, labda Nguzo ile ile ya Moto iliyomwongoza Musa kupitia nyikani, na wana wa Israeli. Kutoka kwenye Nuru hii, labda angavu kuliko nuru ya jua, alikuja Malaika Mkuu Gabrieli, Naye akasema, “Salamu, Mariamu,” kwa maneno mengine, *simama*, “umebarikiwa kati ya wanawake, kwa kuwa umepata kibali kwa Mungu.”

¹¹⁰ Loo, ni salamu za jinsi gani! Ilimtisha maskini yule mwanamwali. Ingekutisha wakati Malaika...

¹¹¹ Mtu fulani aliniambia, “Ndugu Branham, unapomwona huyo akitokea, yeye ni nani?”

Nikasema, “Sijui, kamwe sikuuliza jina lake, ninaogopa sana anapozungumza.”

Unasema, “Vema, mimi ningalimwuliza.”

¹¹² La, usingemwuliza, huwezi kuwazia chochote, unasimama tu kimya.

¹¹³ Loo, jinsi alivyojisikia, akiwa na ndoo yake, akienda kisimani kuchota maji, na hapo njiani alikuwako yule Malaika amesimama pale na kumwambia amepata neema machoni pa Mungu!

¹¹⁴ Ndipo akaanza kumsimulia hadithi, akasema, “Unamkumbuka binamu yako, Mariamu? Jina lake ni Elisabeti, yeye ni mke wa Zakaria, kuhani.” Na wakati Zakaria, yule kuhani, alipokuwa mzee na mkewe alikuwa mkongwe, ila walikuwa watumishi halisi wa Bwana, walikuwa walingojea faraja ya Israeli, kule Kuja kwa Masihi.

¹¹⁵ Mnaona, Mungu ana masalia mahali fulani, mtu fulani anakesha na kungojea, daima amekuwa, daima atakuwa hivyo. Walikuwa wakikesha siku baada ya siku, na walishika amri zote za Bwana. Lakini Elisabeti alikuwa tasa, hakuwa na watoto.

¹¹⁶ Siku hizo ilikuwa ni aibu kutokuwa na watoto, sasa ni fedheha kuwa na watoto. Imebadilika, afadhali ununue mbwa mdogo na kumpa upendo wa mtoto, na kumtembeza kote, na kumbeba kwa gari, na loo jamani! Hmm! Kitu hicho kinachonuka! Unampapasa na kucheza naye, kisha unamwandalia bakuli la biskuti. Siamini hilo, nitawaambia hilo sasa hivi. Mbwa ni sawa, lakini mahali pake ni nje kwenye banda, si ndani ya nyumba. Kwa hiyo basi, kwa vyovyote vile, nitawaudhi sasa nispokuwa mwangalifu, kwa hiyo... Vema, hata hivyo, tuachane na hilo. Zaidi sana, labda hayo ni maoni yangu mwenyewe.

¹¹⁷ Lakini alikuwa akitaka kupata mtoto, naye mumewe alikuwa mzee, naye alikuwa amepita umri wa kuzaa. Nalo agizo la Zakaria hekaluni lilikuwa ni kufukiza uvumba wakati watu walipokuwa wakiomba. Basi wakati alipokuwa akifukiza uvumba, upande wa kuume wa madhabahu akaja Malaika, Gabrieli. Hivi mliona, katika Maandiko katika Luka pale, inasema, “Upande wake wa kuume,” upande wa kuume wa madhabahu.

¹¹⁸ Ukipata kuona moja ya ibada zangu za uponyaji, ninawaleta watu kutoka upande wangu wa kuume kwa sababu Malaika wa Bwana sikuzote huja upande wangu wa kuume. Ninamtaka

akutane na watu, ili wapate upako wanapokuja hapa apate kuwaambia na kuwabariki.

¹¹⁹ Malaika wa Bwana alisimama upande wa kuume wa madhabahu, naye akasema, “Zakaria, Mungu amejibu maombi yako.”

¹²⁰ Mnaona Malaika anakuja kwenye nyumba ya namna gani? Nyumba inayotii amri za Mungu, makazi ya watu wanaotembea kwa unyofu mbele za Mungu. Kama ukitaka heshima ya Malaika kuitembelea nyumba yako, iweke nyumba tayari apate kutembea, iliyoandaliwa na tayari chini ya Damu ya Mwana-Kondoo. Malaika wa Bwana huja mahali kama hapo.

¹²¹ Angalia, huwezi kutembea pamoja na ulimwengu na kumtarajia Mungu kutembea pamoja nawe. Malaika hawatakuzuru, wala chochote kile, ila ulimwengu, kwa sababu huwezi kuchanganya Mungu na ulimwengu pamoja, hawatachanganyikana. Mungu ni mtakatifu, ametenganishwa na ulimwengu.

¹²² Na njia pekee atakayopata kukuona ni wakati anapoangalia kupitia kwa ile Damu, kama nilivyosema hivi majuzi asubuhi, nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe. Yeye hawezi kuangalia kupitia kanuni ya imani, hawezi kuangalia kupitia dhehebu, hawezi kuangalia kwa kupeana mikono, ama maji, hana budi kuangalia kupitia kwenye ile Damu, na anapoangalia kupitia kwenye Damu, dhambi zako nyekundu zinaonekana nyeupe Kwake. Damu ya Yesu Kristo husafisha dhambi zote. Hiyo ni:

Loo, huo mtiririko ni wa thamani,
Unaonifanya mweupe kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Hakuna chochote ila Damu yake Yesu.

Kama vile Eddie Perronet alivyoandika:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!
Malaika na wasujudu;
Leteni taji ya kifalme;
Mkamtawaze kuwa Bwana wa wote.

¹²³ Kwa sababu alikuwa Ndiye pekee, Mtawala pekee, Mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu, hakuna kitu kingine kitakachopachukua mahali hapo, Damu Yake ndiyo kitu pekee kitakachofanya upatanisho, ndiyo Njia pekee ya Mungu, Yeye ndiye Mpatanishi pekee, wa pekee—wa pekee ni kupitia kwa Yesu Kristo.

¹²⁴ Sasa, niko kwa Zakaria, chini ya damu iliyomwagika ya mwana-kondoo, nimesimama pale. Naye akasema, “Baada ya siku hii hapa, mimi ni Gabrieli, nisimamaye Mbele za Mungu,” naye akasema, “unaenda nyumbani, naye mke wako atachukua mimba, atamzaa mwana, utamwita jina lake Yohana. Atakuwa

mkuu, naye ataigeuza mioyo ya wana wa Israeli irudie amri za Mungu.”

¹²⁵ Halafu basi, wakati Zekaria, liwazieni sasa, mhubiri, kuhani hekaluni, amesoma Maandiko, mifano mingi sana kwamba jambo kama hilo lilikuwa limetukia hapo kabla, Hapo alikuwapo Hana mwanamke ambaye hangeweza kupata mtoto naye Mungu akampa mtoto, kulikuwako na Sara, akiwa na umri wa miaka tisini, Mungu alimpa mtoto, hayo yalikuwa yametukia hapo kabla, lakini yeye alilihoji, akasema, “Jambo hili lingewezekanaje? Mke wangu ni mkongwe, nami ni mzee, basi ingewezekanaje?”

¹²⁶ Yule Malaika akanena upesi, na kusema, “Maneno yangu yatatimizwa katika siku zake, lakini kwa sababu hukunisadiki, hukulisadiki neno langu, utakuwa bubu hata siku huyo mtoto atakapozaliwa, lakini maneno yangu yatatimizwa.”

¹²⁷ Haleluya! Mungu hutimiza Neno Lake, halibadiliki. Kama kanisa hili la Kipentekoste likikataa kumsifu Mungu, Mungu angeweza kuwainua Wamethodisti, Wabaptisti, ama kitu kingine kumsifu. Kama kanisa la Kipentekoste likiukataa Ujumbe wa Mungu, Mungu anaweza kuwachukua Wakatoliki, wakanamungu, makafiri, ama chochote kile, na kujiinulia Mwenyewe Jina. Na, Neno la Mungu litatimizwa.

¹²⁸ “Kutakuwako na nyakati ambapo Roho atamwagwa kutoka Juu. Kutakuwako... Vijana wataona maono, wazee wataota ndoto. Hapo nitawamwagia watumishi Wangu wanaume kwa wanawake Roho Yangu, nikionyesha ishara katika mbingu juu.” Na mambo haya yote yaliyonenwa yatatimia, Mungu alisema hivyo. Amina.

¹²⁹ Mkitaka kuwa na mfano wa utauwa, mkane nguvu zake, endeleeni, huko ni kutimiza Maandiko, lakini Mungu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watahika nyoka, ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mtu fulani, mtu fulani atafanya hivyo. Neno la Mungu halibadiliki. Hiyo ni kweli.

¹³⁰ “Neno langu litatimizwa, kwa sababu mimi ni Gabrieli nisimamaye Mbele za Mungu, bali utakuwa bubu wala huwezi kuzungumza tena, kwa sababu umetilia shaka. Wala kamwe hutaweza kufanya hivyo, mpaka siku ile mtoto huyo atakapozaliwa.”

¹³¹ Halafu basi, Malaika huyu alijua hilo, Malaika yuyu huyu, miezi sita baadaye, alitumwa kwa maskini Mariamu na kumwambia habari zake miezi sita baadaye. Sasa, maskini Mariamu alisema... Sasa, kamwe hakusema... hakumhoji, alisema tu, “Itakuwaje, maana sijui mume?”

¹³² Akasema, “Roho Mtakatifu atakutia uvuli.” Loo, napenda hilo! “Roho Mtakatifu atakuja juu yako, nawe utachukua mimba

tumboni mwako na kumzaa Mwana, bila kumjua mume yeyote. Lakini Mwana huyu atakuwa ni Mwana wa Mungu, Naye atawaokoa watu Wake na dhambi zao. Naye atakitwaa kiti cha enzi cha baba Yake, Daudi, Naye atamiliki milele na milele, wala amani haitakoma kamwe.”

¹³³ Nena kuhusu amani? Wanasema, “Vema, Yeye alikuwa Mfalme wa Amani.” Naam, na kila mtu anayemkubali Yeye anayo amani ya Milele moyoni mwake.

¹³⁴ Huenda ulimwengu ukawa vitani, na huenda kukawa na vita katika kusema jambo hili, Yeye kamwe hakusema *ulimwengu* ungekuwa hivyo. Falme za ulimwengu huu ni za ibilisi, kila moja ya hizo unatawaliwa na ibilisi.

¹³⁵ Biblia inasema ya kwamba Marekani hii, na ulimwengu mwingine wote unatawaliwa na ibilisi, hiyo ndiyo sababu tunapigana na kuendelea. Lakini wakati Yesu atakapokuja na kuketi kwenye kiti cha enzi cha baba Yake, Daudi, amani kamilifu itatawala katika kila moyo. Ee Mungu, siku hiyo na ije!

¹³⁶ Wakati Shetani alipompandisha juu, na kusema, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, fanya *hivi*. Na ukiwa ndiwe...” Akamchukua kumwonyesha falme za ulimwengu, falme zote zitakazokuwako, kasema, “Hizo ni zangu, ninazifanyia nitakayo, nitakupa wewe, kama utainama na kuniabudu.”

¹³⁷ Yesu alijua katika ule Utawala wa Miaka Elfu angeurithi huo, Yeye akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani, kwa maana imeandikwa, ‘Msujudie Bwana, Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake.’”

¹³⁸ Loo, jamani! Sijui kwa nini nasumbuka. Naitakia heri nchi yetu. Hakika, ninaamini hilo, viongozi wetu, na mambo kama hayo, bali ingali inatawaliwa na Shetani, Biblia inasema hivyo. Mambo haya yote ya kuvua nguo yanayoendelea mnayosikia habari zake, kumbukeni tu, ndugu, tunautazamia Mji ujao ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu. Hiyo ni kweli. Tunautazamia Ufalme ujao, si Ujerumani, si Uswisi, si Marekani, ni Kristo na Ufalme utokao Juu.

¹³⁹ Yesu alisema, “Kama Ufalme Wangu ungalikuwa ni wa dunia hii, basi ningewafanya watu Wangu wanipiganie, lakini Ufalme Wangu uko Juu. Nami ningeweza kumwita Baba Yangu na mara Yeye angenipa majeshi ishirini ya Malaika.” Amina! Wakati Malaika mmoja angeweza kuuangamiza ulimwengu mzima.

Usiutamani utajiri wa bure wa ulimwengu
huu,
Unaoza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hayatapita kamwe!

¹⁴⁰ Vita hivi, tunawapeleka watoto hawa wadogo huko nje, walio bora kabisa, maana hawajui kitu ila kujua nidhamu, nidhamu ya

jeshi, “Chomoza kichwa chako juu ya kilima na kumwacha mtu fulani akipige risasi kichomoke, ufe kama shujaa.” Wanafanya hivyo kwa furaha. Wanakimbia kule juu na mmoja anapigwa risasi, mwingine anapigwa risasi, mwingine anapigwa risasi, taifa linawasahau ila familia yao tu. Wanarudi kwenye hili hapa, na chochote watakachorudia . . . mnaona ninalomaanisha, wengi wa hao askari.

¹⁴¹ Lakini mtu, ni kwa nadra sana kumwona mtu ambaye atayatoa maisha yake kwa ajili ya Kristo. Hata hatatambaa kutoka kwenye mti wenye kivuli aende kanisani, hata hatatoka nyuma ya televisheni muda mrefu kutosha kuhudhuria mkutano wa maombi wa Jumatano usiku. Hiyo ni kweli. Amina. Ni aibu, fedheha.

¹⁴² Hiyo ndiyo sababu Malaika hawatembelei makanisa, hiyo ndiyo sababu Malaika hawatembelei makazi. Hatuna budi kuingia kwenye uaminifu wa kina wa jambo hili. Malaika wa Mungu wako humu duniani usiku wa leo, kama tu vile walivyokuwa sikuzote.

¹⁴³ Roho Mtakatifu amekuwa hapa tangu kufufuka Kwake Yesu Kristo na kuja kwa Pentekoste. Ameonekana kote katika nyakati, akikusanya masalia ya watu pamoja, hao wengine ni chakula cha mzinga, nitawaambia tu hilo sasa. Ni chakula kitakachofanyiza moshi kutoka matesoni. Naam, bwana. Itahitaji tukio la kuzaliwa mara ya pili, kuoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo, kutakaswa, kujazwa na Roho Mtakatifu, la sivyo kamwe hawataupata huo Unyakuo, kulingana na Neno hili. Naam. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo hasa.

¹⁴⁴ Msichana mmoja hapa Oregon alikuwa akijaribu kujadiliana nami wakati mmoja, alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo Mary alikuwa ndiye bosi wake, naye akasema, akizungumzia ninii, kasema, “Ningechukia kujua ya kwamba ningeninii. . .” Kasema, “Unataka kuniambia ya kwamba wakati wa ninii. . . Mbinguni ambapo kundi hili la wapumbavu kama wale waliokuwa wakipiga makelele huko juu jana usiku ambako ulikuwa ukihubiri, ati hao ndio watu watakaokuwa wanatawala Mbinguni?”

¹⁴⁵ Nikasema, “Hivyo ndivyo Biblia inavyosema.” Akasema. . . Nikasema, “Bikira Mariamu mbarikiwa wako, ilibidi apande kwenda Pentekoste na kumpokea Roho Mtakatifu, na kutenda kama hao watu walivyofanya jana usiku, la sivyo hangalienda Mbinguni kamwe.”

Akasema, “Hivyo sivyo!”

¹⁴⁶ Nikasema, “Hebu nikuonyeshe papa hapa katika Matendo 2 kama ndivyo ama sivyo. Mariamu alilewa sana akayumbayumba kana kwamba alikuwa, amelewa kwa Roho, na kutenda kama mlevi kwenye Siku ya Pentekoste. Na kama Mungu

hangemwacha Mariamu aende Nyumbani Mbinguni na chochote pungufu ya hilo, utafanikiwaje bila hilo?" Hiyo ni kweli. "Hebu uwe mfuasi wa kanisa lolote utakalo, itakubidi kuwa na tukio lile lile, jambo lile lile, hasa."

Akasema, "Vema, si—si—singetaka kuwa kule."

¹⁴⁷ Nikasema, "Sidhani inakubidi kusumbuliwa sana na hilo." Uh-huh. Hiyo ni kweli. "Sidhani una mengi sana ya kujisumbua nayo." Nikasema, "Sasa endelea ukaandike makala yake machafu sana gazetini, nami nitakwambia hili: BWANA ASEMA HIVI, yazingatie maneno yangu, kati ya huu na miezi miwili kuanzia sasa, ukifa kando ya barabara katika ajali, utakumbuka maneno niliyokwambia."

¹⁴⁸ Wala hakuandika chochote. Hiyo ni kweli. Alifanya ujanja wa busara pale. Nilimwona akifa, amelala katika ajali ya motokaa. Mungu alikuwa akimpa nafasi wakati huo, bali alikuwa mwerevu vya kutosha kutoandika chochote, hakukuwako na chochote gazetini, waliyaachilia tu, kwa hiyo hilo ndilo wazo la busara. Aliokoa tu maisha yake mwenyewe kwa hilo. Mnaona, Mungu angali ni Mungu.

¹⁴⁹ Mungu alisema, "Ni afadhali ufungiwe jiwe la kusagia shingoni mwako ukazamishwe katika vilindi vya bahari hata kumkosesha mmojawapo wa watoto hawa waniaminio Mimi." Ni kitu gani hicho?

¹⁵⁰ Vema, unasema, "Vema, mimi ni mtu mdogo aaminiye."

¹⁵¹ Biblia inasema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Mungu hupambanua, Yeye huwapa watu alama. "Akiamini, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hiyo ni kweli, mwaminio, si wasemao wanaamini, si anayedhaniwa kuwa mwaminio, bali mwaminio halisi.

¹⁵² Ninataka kuwa mfuasi wa kanisa ambalo lina ishara na maajabu yanayolifuata, hapo ndipo ninapotaka kufanya ushirika wangu, papo hapo chini ya Damu ya Yesu Kristo. Ambapo Malaika, na nguvu, na Roho Mtakatifu, na Mungu hufanya kazi huku na huku kupitia Kanisa Lake, kupitia kwa watu Wake, akionyesha ishara na maajabu.

¹⁵³ Mbona, ndilo jambo kuu sana nililopata kujua maishani mwangu! Ni sehemu ya Mbingu duniani, watu watakaolichukua Neno la Mungu. Kama huna Roho Mtakatifu ndani yako, unaweza je kuchukua Neno la Mungu? Roho Mtakatifu aliye ndani yako atasema, "Amina," kwa kila Neno aliloandika Mungu. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁴ Kama—kama Biblia ilisema, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele," ninii. . . kama una Roho ndani yako atasema "Amina." Kama Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," na kanisa lenu lilisema hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine, Roho Mtakatifu aliye ndani yako atasema,

"Amina. Neno la Mungu ni kweli. Neno la kila mtu mwingine ni uongo."

¹⁵⁵ Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana, Mungu wetu, wamjie."

Nalo kanisa lako linasema, "Roho Mtakatifu alikoma huko nyuma kwa mitume."

Utasema, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na la Mungu liwe kweli." Amina.

¹⁵⁶ Roho Mtakatifu atakubaliana na Neno Lake Mwenyewe. Ni kwa ajili *yako* na kwa ajili *yako* na kwa kila kiza... mradi tu Bwana anaita, Roho Mtakatifu angali yuko kumbatiza kila mtakatifu na kila mwaminio. Amina. Neno la Mungu lisilobadilika!

¹⁵⁷ Basi nilikuwa nikihubiri hivi majuzi usiku lile la *Kwa nini?* Maandiko, ama, kile kifungu cha *Kwa nini? Kwa nini?* Mungu atauliza, "Kwa nini?" Utatoa hesabu kwa ajili yake. "Je, hakuna zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?"

¹⁵⁸ Mtakatifu Petro aliandika, alikuwa Dk. Simoni Petro, aliandika hayo maagizo kwenye Siku ya Pentekoste. Mnaamini hilo? Waliposema, "Waume na ndugu zetu, tufanye nini?" aliandika Maagizo kwa ajili ya Zeri.

¹⁵⁹ Usijaribu kujipumbaza nayo, usijaribu kutoa kitu kutoka kwake, useme, "Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu."

¹⁶⁰ Hebu chukua baadhi ya hawa wauza dawa bingwatapeli ambao wangechukua, ama daktari bingwatapeli ambaye angechukua ma—maagizo ambayo daktari halisi alikuwa ameandika ambayo yangeponya ugonjwa, naye daktari bingwatapeli au mwuza dawa achukue kitu kutoka humo, ni kitu gani? Mle ndani, mna sumu nyingi, na kuna sumu ya kutosha kuua kijidudu, kiuasumu cha kutosha kuizuia isikuue. Kama ungekunywa kiuasumu chote, sumu hiyo ingekuua, utamwua mgonjwa wako.

¹⁶¹ Hiyo ndiyo shida ya mengi ya makanisa haya siku hizi, ya kawaida sana na maovu, wanaliua kanisa lao kwa kuchukua maagizo na kuunda kitu fulani, fundisho la sharti kutoka kwake, na kutoyaacha jinsi Mungu alivyoyaandika. Haleluya! Ninaamini Neno la Milele la Mungu ni halisi tu kama lilivyowahi kuwa. Nililithibitisha tena, na tena, na tena, na tena, nami ninajua ni la kweli. Amina.

¹⁶² Zakaria alikaa papo hapo jukwaani, naye Malaika akamwacha, ndipo akawa bubu.

¹⁶³ Sasa, yule Malaika akasema, “Binamu yako, Mariamu, tayari ana miezi sita, kama ilivyo desturi ya mama.” Kisha kasema, “Sasa, Kitu hiki Kitakatifu kilichozaliwa ndani yako, kitakuwa ni Mwana wa Mungu.”

¹⁶⁴ Mnajua yale Mariamu aliyosema? Laiti tungalikuwa na akina Mariamu zaidi hapa sasa. Mariamu alisema, “Tazama, mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu sawasawa na Neno Lako.” Loo, jamani!

¹⁶⁵ Kamwe hakuhoji, hakuhoji kamwe. Na isitoshe, hakungojea mpaka alipohisi uhai, hakungojea mpaka alipokuwa na uhakika, hakungojea mpaka angeona ya kwamba kitu fulani kimekoma kwake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁶⁶ Utukufu! Hilo ni zuri vya kutosha. Mungu anaposema hivyo, hilo latosha Milele. Neno hilo lilikuwa zuri vya kutosha kwake, akasema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu sawasawa na neno lako,” kisha akaanza kulifurahia, si kungojea. Mnaona, ilimbidi kuamini yasiyowezekana, ilimbidi kuamini jambo ambalo kamwe halikutukia. Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya, hatuna budi kuamini yasiyowezekana tupate kuona Uzima mpya. Amina.

¹⁶⁷ Lakini unapoamini yasiyowezekana! Kama daktari akisema una kansa nawe unakufa, huna budi kuamini yasiyowezekana upate kuona uhai mpya ukikushika. Amina. Kama daktari akisema kamwe hutatembea, huna budi kuamini kisichowezekana upate kuona uhai mpya ukiingia ndani yako, uhai mpya katika nyuzinyuzi hizo. Na, Ee Mungu, ulete mkono mpya, mkono mpya, mapafu mapya, tumbo jipya, chochote kile, Mungu atafanya hivyo, kama utaamini Neno Lake.

¹⁶⁸ Sasa, yeye hakuwa na ushahidi wa jambo hilo hata kidogo, neno lake tu. Loo, napenda hilo! Nafikiri sasa hivi, tulieni kwa dakika moja tu. Kama nilivyosema, simhubirii kila mtu anayeishi moja kwa moja kwenye barabara kuu, inanibidi nishuke kwenye uchochoro wakati mwingine kumwokota mtu fulani.

¹⁶⁹ Kumbukeni yule kahaba, Rahabu. Yeye hakuninii... Loo, wakati wale wapelelezi walipoleta taarifa kuhusu Yoshua kuwa mtu mashuhuri wa Mungu, naye Mungu alikuwa amemwambia jinsi, “Nitakuwa pamoja nawe kama nilivyokuwa pamoja na Musa,” alikuwa amesikia jinsi Waamori wote, na kadhalika, huko chini walivyokuwa wameathirika, na jinsi alivyokuwa amemwua Agagi, na kadhalika, Musa alikuwa amemwua, bali kamwe hakusema, “Ngojeni kidogo mpaka nitakapomwona Yoshua, na hebu nimwone akifanya namna fulani ya muujiza, ndipo nitaamini.” La, bwana. Neno la wapelelezi lilikuwa zuri vya kutosha kwake. Haleluya!

¹⁷⁰ Akawa nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya wa Bwana wetu Yesu Kristo, pia. Hiyo ni kweli kabisa. Aliolewa na a—

afisa kutoka Israeli, na kutoka kwa huyo akaja mwana ambaye alikuwa Boazi, na kutoka kwa Boazi akaja Yese, kutoka kwa Yese akaja Daudi, kutoka kwa Daudi akaja Mariamu. Haleluya!

¹⁷¹ Kwa nini? Mmataifa, asiyetahiriwa moyo wala masikio, aliuamini Ujumbe na kuupokea bila ushahidi wowote hata kidogo. Alisikia ya kwamba kulikuwako na Mungu aliyekuwa...

¹⁷² Loo, ninajisikia kubarikiwa! Aliamini Ujumbe, aliamini Neno la Mungu, jina lake halipatikani na mauti. Mama wa nyanya ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwa sababu aliamini Neno la Mungu. Basi angalia alikolazimika kutoka, akiwa ni kahaba mjini.

Loo, ni kitu gani kinachoweza kuosha dhambi zangu?

Hamna ila Damu Yake Yesu;

Ni kitu gani kinachoweza kunifanya mzima tena?

Hamna ila Damu Yake Yesu.

Loo, mtiririko huo ni wa thamani

Unaomfanya kahaba mweupe kama theluji;

Sijui chemchemi nyingine,

Hamna ila Damu Yake Yesu.

¹⁷³ Hakuna kanisa, hakuna kanuni ya imani, hakuna dhehebu, hakuna *hili*, hakuna *lile*, Damu ya Yesu Kristo tu ndiyo yote itakayokufanya mweupe. Amina. Sasa, siyabishanii makanisa yenu, siibishanii kanuni yenu ya imani, Ninajaribu kusema, “Usiweke matumaini yako juu ya hilo.”

Usiseme, “Mimi ni Mmethodisti na hilo latosha.”

¹⁷⁴ Kama wewe ni Mmethodisti, na umeoshwa katika Damu ya Yesu Kristo, na kujazwa na Roho Mtakatifu, Mungu aubariki moyo wako, sisi hakika ni asilimia mia moja ndugu na dada. Naam, bwana. Mbaptisti, Mpresbiteri, Mkatoliki, Mlutheri, chochote uwezacho kuwa.

¹⁷⁵ Lakini unaposema, “Vema, mimi ni Mmethodisti,” “Mimi ni Mbaptisti,” hilo halimaanishi chochote. Yesu alisema haikuwa hivyo tangu mwanzo. Hiyo ni kweli. Hajui chochote kingine ila Damu Yake Mwenyewe.

¹⁷⁶ Mungu hatatambua kitu kingine ila Mwanawe Mwenyewe. Na hiyo ni kweli. Yeye, “Huyu ni Mwanangu mpendwa,” Mungu alisema kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, “Msikieni Yeye.” Amina.

¹⁷⁷ Yesu alisema, “Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Juu ya Mwamba huo ninasimama usiku wa leo, haidhuru ninajisikiaje, ama yale ibilisi asemayo. Sawa.

178 Neno la Mungu: “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitapita kamwe.” Amina. Ninatumaini Neno Lake, hakuna kitu kingine ni juacho ila Neno Lake, Hilo ndilo ninaloamini.

179 Na mimi—mimi siendi jinsi ninavyojisikia, ibilisi hufanya, angenifanya nijisikie wakati mwingine sikuwa nimeokoka, pia ibilisi ananifanya nijisikie sikuponywa, sijali anachosema, ninaweza kumshinda kwenye Neno hilo kila wakati. Ninasema, ni “BWANA ASEMA HIVI. Angalia Hilo, jamani! Naam, bwana, huwezi kuliondoa Hilo.”

180 Yesu alimshinda vivyo hivyo, Yeye alisema, “Imeandikwa!” Alikuwa na mamlaka ya kumrudisha kuzimuni, bali hakufanya hivyo. Alionyesha ya kwamba Shetani angeweza kushindwa papo hapo kwenye Neno la Mungu. Yeye, kila wakati Shetani alipokutana Naye, Yeye alimshinda kwa Neno la Mungu. Neno la Mungu la Milele, la dawamu ni la kweli. Naam. Amina. Ninapenda hilo. Jua ya kwamba una msingi imara.

181 Hakungojea kitu kingine chochote, aliweka Neno la Mungu moyoni mwake, naye alikuwa akizunguka huku na huku akishuhudia ya kwamba atapata Mtoto kabla hajawa na ushahidi wowote wa jambo hilo ama la. Sasa angalieni, kwa mwanamke kijana kupata mtoto bila kuolewa, hiyo ingekuwa ni aibu. Yeye hakujali kuhusu aibu, alikuwa na Neno la Mungu.

182 Watu wengi sana usiku wa leo wanasema, “Loo, kama ingenibidi kushuka kule chini na kupiga makelele *woo-hoo* na kulia, kama ingenibidi kunena kwa lugha hizo, loo, si mimi! Loo, mbona, mama yangu angenifukuza. Jamii yangu, mbona, kamwe wasingecheza karata pamoja nami tena.”

183 Usijali, ukifanya hivyo, hutacheza karata zingine tena, kwa vyovyote vile, hiyo ni kweli, kwa hiyo haikubidi kuwa na wasiwasi kuhusu hilo. Na mashirika yenu yatakuwa ni lundo la takataka kwako, hiyo ni kweli kabisa, maana kutakuwa na jamii moja tu, hiyo ni Damu ya Yesu Kristo, na Waliokombolewa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, haleluya, hiyo ndiyo jamii ya Yesu Kristo. Amina. Walioosha kwa damu, wanaosengenywa, kudharauliwa, kukataliwa, kutupwa nje, kuitwa wapumbavu, kila kitu kingine, lakini hilo haliondoi ahadi ya Mungu. Mungu anabaki yeye yule jana, leo na hata milele. Wala hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake, nalo Neno Lake linadumu likiwa tu vilevile sasa kama lilivyowahi kuwa kwa kila mtu atakayeliadini.

184 Akasema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu sawasawa na Neno Lako.” Ninaweza kuona macho yake madogo ya hudhurungi yakiangaza, kama nyota za mbinguni.

185 Yeye akishuka kwenda kote akisema, “Mnajua, nitapata Mtoto?”

“Loo, Mariamu!”

“Naam, nitapata Mtoto.”

“Kwani wewe na Yusufu mmefunga ndoa?”

“La! Atakuwa ni Mwana wa Mungu.” Amina.

¹⁸⁶ Hakuna kitu kama hicho kilichowahi kutukia hapo kabla. Bali hakujali kama kiliwahi kutukia hapo kabla, kwa vyovyote vile, alikuwa na Neno la Mungu, ahadi ya Mungu, hilo lilikuwa zuri vya kutosha. Hakujali kuhusu sehemu yake ya aibu, alikuwa na Neno la Mungu kwa ajili yake, hakika.

¹⁸⁷ Angalieni hekaluni siku ile alipomweka wakfu, huyu hapa anakuja, na akina mama wote wakikaribia, wamewavalisha hao watoto wachanga hizo nguo ndogo zilizoshonwa kwa sindano, na vitu kama hivyo, na—na hapo wote walisema, “Uh-loo! Angalieni *pale*, yule pale Mariamu. Mnaona, mtoto huyo alizaliwa nje ya ndoa, kaeni mbali naye, kaeni mbali,” nao wakakaa mbali sana na Yeye.

¹⁸⁸ Alikuwa amefungwa nguo za kitoto, si za kushonwa, nguo za kitoto. Basi wakati alipokuwa amelala mle ndani... Kama nimeambiwa kweli, hizo ni nira juu ya maksai wanazoziweka zizini mle ndani, kwamba walikuwa na kitu kilichozizuia kukwaruza bega lake, wanadai hicho ndicho Yesu alichofunikwa, hata hakuwa na nguo za kuvaa, hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake, alikuja duniani kupitia tumbo la uzazi lililoazimwa juu ya lundo la samadi, akatoka na ikambidi kuazima kaburi la kuzikiwa. Na halafu tunafikiri sisi ni *mtu fulani*. Loo jamani!

¹⁸⁹ Mungu wa Mbinguni ambaye angeweza kuumba mkate na samaki, na kugeuza maji yakawa divai, Yeye aliyeumba Mbingu na nchi, na kupachukua mahali pa mtu mnyenyekevu, fukara kuliko wote, akatawadha miguu ya wanafunzi, mavumbi yenyewe aliyumba akayatawadha. Mavumbi yaleyale hasa aliyumba Yeye alifanywa kwayo, akaweka hema Lake hapa chini, na kuishi miongoni mwetu katika mwili wa nyama, akavuka tabaka Lake, akashuka kutoka kwa Mungu Mbinguni, akawa Mwanadamu kusudi auguse moyo, hiyo ni ishara kuu.

¹⁹⁰ Ni ishara halisi. Nena kuhusu ishara: wakati Yehova alipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, ishara ambayo inapaswa kuugusa moyo wa kila mtu kujua ya kwamba Mungu ni mnyenyekevu sana. “Mungu, wa thamani, mpole, aliweka kando fahari Yake, akainama apate kuishawishi, na kuiutia nafsi yangu.” Kama vile Booth-Clibborn alivyoandika ule wimbo maarufu, *Alishuka Kutoka Utukufuni Mwake*. Loo, jamani, jinsi ninavyopenda kuusikia huo ukiimbwa Utukufuni! “Yule Muumba mkuu akawa Mwokozi wangu. Nao utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.” Jinsi ninavyopenda huo!

¹⁹¹ Katika siku hizi wanapojaribu kumfanya nabii, wanapojaribu kumfanya mwanadamu tu, Yeye alikuwa zaidi ya hilo, alikuwa Imanueli.

¹⁹² Huyo hapo. Alipotoka mbio, na kuanza kumwambia kila mtu kile kilichokuwa kimetukia, loo, jinsi Mungu alivyokuwa amembariki, basi ilitokea akawazia, “Elisabeti, binamu yangu, sijamwona kwa miaka mingi, kwa hiyo nitafikiri nitaponyoka niende kumwona.”

¹⁹³ Kwa hiyo akakimbia kwenda kumwona, kama nilivyosema hivi majuzi usiku. Basi alipofika kule kumwona, alikuwa amejificha siku kadhaa, kwa sababu alikuwa, hawakujianika wakati huo kama wanawake wafanyavyo sasa. Na kwa hiyo, alikimbia mahali fulani na kujificha huko nyuma.

¹⁹⁴ Waangalieni kina mama hawa (Samahani, akina dada, tafadhalini, hebu kidogo, wekeni tu dhamiri zenu kando kwa dakika moja. Ninyi humsikiza daktari wenu, ninapaswa kuwa vile vile, mimi ni ndugu yenu.), bali mwanamke akiwa hapa nje na ni mja mzito, akizunguka-zunguka mtaani, maskini hizo kaptura, na vitu kama hivyo, ni fedheha kwa taifa, kwa bendera, kwa jamii ya binadamu, kwa chochote kile. Sigara mkononi mwake akitembea namna hiyo, loo, jamani, jamani, jamani!

¹⁹⁵ Kama—kama huyu niliye naye ni Roho Mtakatifu, mtakuwa na nafasi ndogo sana ya kufika hata mlangoni. Na hiyo ni kweli. Mungu anachukia hilo. Naam, bwana. Hilo ndilo jambo duni kuliko yote alilopata kufanya mwanamke, wakati alipoanza kuvuta sigara. Nanyi waume mtakaomwacha afanye hivyo, vema, nina maoni yangu kuwahusu. Hiyo ni hakika. Wewe si bosi wa nyumba yako, la hashu.

¹⁹⁶ Sisemi mke wangu hatafanya hivyo, lakini atakapofanya hivyo, hatakuwa Bibi William Branham, hilo litakuwa jambo moja la hakika. Naam kweli, sisemi binti zangu hawatafanya hivyo. Lakini hebu angalieni tu mgongo wao mwone ni malengelenge mangapi yaliyo juu yao tukimalizia. Hiyo ni kweli kabisa. Sisemi hawatafanya hivyo, sijui, Mungu anashikilia ya usoni, natumaini sitazaa kitu kama hicho, hiyo ni kweli, sijui yatakatukia.

¹⁹⁷ Lakini sikilizeni, wakati... Kibaraka msaliti mbaya kuliko wote aliyepo hapa nchini ni mama anayevuta sigara. Ninapata takwimu kutoka serikalini, inasema ya kwamba asilimia themanini ya akina mama wanaovuta sigara inawabidi kuwanywesha watoto wao maziwa ya ng’ombe iwapo wanavuta sigara. Kama wakinywa sumu ya nikotini kutoka kwenye hayo maziwa, hawaishi miezi kumi na minane. Wazia hilo. Hujuma? Loo, kama ambavyo nimesema kila mara, “Robini anayelidonoa tofaa siye anayelidhuru, mdudu aliye kwenye kiini chake ndiye anayeliua.” Hiyo ni kweli, ni uchafu na kinyaa chetu wenyewe kilichotuzunguka.

¹⁹⁸ Haya makampuni ya sigara hujaribu na kuwafanya wanawake wafikiri wanapunguza, inakupa TB na kansa. Hivi madaktari hawawaambii hivyo? Usisikilize haya yote. Jinsi

wanavyochukua kitu hicho na—na kukiweka huko nje kwenye televisheni, na—na kisha kuifutilia mbali katika kodi za serikali ya Marekani, kisha wamchukue mhubiri na kumtupa gerezeni kwa kutolipa kodi kwa *kitu fulani*, anawekwa ndani. . . Loo, jamani! Tumeiva kwa ajili ya hukumu, hakuna kilichosalia ila hukumu. Sawa.

¹⁹⁹ Halina umri mkubwa sana, Ufunuo 13 ilisema taifa hili halitaishi muda mrefu sana, hata hivyo, mnajua hilo. Maskini yule mwana-kondoo aliinuka, wala kamwe hakuwa kondoo dume kama hao wengine, alikufa katika ujana wake. Hiyo ni kweli. Wakati mamlaka ya kikanisa na mamlaka ya serikali yalipokutana pamoja na hizo pembe mbili ndogo za kondoo dume kisha yakaliunganisha kanisa na taifa, na karibu tunafanya hivyo sasa hivi, inategemea tu wimbi linavumia upande gani watakapofanya uchaguzi mwingine. Nasi karibu tumelifikia sasa hivi, acha tu liendelee.

²⁰⁰ Huenda mkafikiri mimi ni mlokole, lakini liandikeni kwenye kipande kidogo cha karatasi mahali fulani, na kukichomeka kwenye Biblia yako, na uangalie moja ya siku hizi, anakuja, huenda yuko papa hapa mlangoni. Afadhali uombe, afadhali uwe sawa na Mungu, ile saa imekaribia!

²⁰¹ Unapooona “Mataifa yakivunjika, Israeli ikiamka, ishara ambazo Biblia ilitabiri; siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu; loo, rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu,” loo, jamani, yaondokeeni mambo haya ya ulimwengu na mumwendee Mungu upesi mwezavyo, Ndilo tumaini pekee tulilo nalo, Kitu pekee kilichosalia. Kila taifa liko tayari kulipuliwa vipande-vipande, wakati wa mwisho umekaribia, wala hakuna kitu kingine kinachoweza kuinuka, hakuna mahali unapoweza kuweka matumaini yako ila juu ya Kuja kwa Bwana Yesu Kristo na haki ya siku Zake. Amina. Jinsi hilo lilivyo kweli!

²⁰² Mariamu akapanda kwenda kukutana na Elisabeti. Nami ninaweza kumwona Elisabeti huko nyuma akishona vijiatu hivi vidogo, mwajua, na kutayarisha vitu kwa ajili ya mtoto huyo mchanga. Lakini mnajua jambo la kigeni lilikuwa, huyo mtoto mchanga hakuwa amesogea kamwe, alikuwa na miezi sita, huyo mama, na hilo kwa jumla si la kawaida, tunajua hilo. Yapata miezi mitatu hadi minne, na hii ni miezi sita na mtoto Yohana hakuwa amesogea kamwe. Naye alikuwa huko nyuma akishona vijiatu. Basi ninasikia baadhi yao wakisema, “Ninamwona mwanamke akija,” labda mtu fulani huko nje.

²⁰³ Ndipo Elisabeti akainua pazia, akaangalia, akasema, “Ninapaswa kumjua mwanamke yule. Yeyote yule, amejaa furaha.”

²⁰⁴ Mnajua, kitu fulani kuhusu Mkristo ni mwenye furaha sana. Kuna jambo fulani kuhusu mtu ambaye amewahi kukutana na

Mungu, kuna kitu fulani chenye furaha kuhusu huyo mwanamke ama mwanamume.

205 Huyu hapa maskini Mariamu anakuja, alikuwa na umri wa kama miaka kumi na minane tu, macho yake madogo yalikuwa yakimetameta, maskini mashavu yake ya waridi, naye huyu hapa anakuja upesi alivyoweza kuja. Loo, alikuwa tu akishangilia na—na kumsifu Mungu.

206 Ndipo alipokaribia, Elisabeti akaangalia vizuri, naye akasema, “Vema, kama huyo si Mariamu, binamu yangu!” Sasa, mnajua ya kwamba Yohana na Yesu walikuwa binamu wa pili. Kwa hiyo, akasema, “Huyu hapa Mariamu anakuja, binamu yangu.” Ndipo akatoka mbio nyumbani, akachukua shela yake ndogo, na kujifunika, akatoka mbio, ndipo akakutana na Mariamu na kumtupia mikono na kuanza kumkumbatia.

207 Mwajua, laiti watu wangependana tena namna hiyo, sivyo? Loo, jamani, wao ni baridi, sivyo? Baridi tu kama chunusi kwenye kachumbari, sijawahi kuona kitu chochote kama hicho maishani mwangu. Loo, ni mbaya sana. Hakuna mtu aliye na urafiki tena.

208 Ndugu Arganbright, unakumbuka miaka mingi iliyopita, wakati tulipokuwa na shamba, na jambo fulani likampata jirani kule, akawa mgonjwa, tungeenda huko na kukata kuni zake, na—na kuingiza mahindi ndani, na kulimia mahindi, ama chochote kile? Tulisaidiana kutunzana, sasa hujui jirani yako amekufa mpaka ulisome kwenye gazeti, ama mahali fulani. Hiyo ni kweli. Hatupendani tena sisi kwa sisi.

209 Nasi tunakuja, kama hapa si muda mrefu uliopita, watu hata hawatendeani mema, nilikuwa nikienda katikati ya mji, atanijutisha hili, mke wangu, kwa hiyo nilikuwa nikienda katikati ya mji, mama huyu akasema, “Halo, Dada Branham.”

Nikamwangalia, nami nikasema, “Meda,” nikasema, “yule mama alizungumza nawe.”

Akasema, “Nilizungumza.”

210 Nikasema, “Alisikiaje, wakati sikuweza kuisikia nikiwa nimeketi hapa? Nami najua masikio yangu ni mazuri, kusikia kwangu ni sawa.” Nikasema, “Ali—alikusikiaje?”

Akasema, “Ni—nilitabasamu.”

Nikasema, “Loo, jamani, maskini tabasamu la kipuuzi!”

211 Sasa, huko si kuzungumza, la, bwana. Ninapenda kupeana mikono kuzuri, kwa mtindo wa kale, wa kupampu namna *hiyo*. Na—napenda kukuhisi.

212 Kama vile Paul Rader alivyosema alipoondoka nyumbani kwake siku moja, alisema yeye na mkewe walikuwa wakizozana kidogo mezani. Nyote mnamkumbuka marehemu Paul Rader,

alifia hapa chini California? Makaburi ya wahubiri, huko Los Angeles, wote huingia humo wakafa.

²¹³ Kwa hiyo basi, walipofika mahali pale, wakati alipoondoka, alisema alimwacha mkewe, nao walikuwa wakizozana kidogo, ndipo kasema, kwa kawaida, mlangoni angeninii, angemuaga kwaheri, atoke nje ya lango, kisha wangepungiana mikono ya kwaheri, kasema asubuhi hiyo alienda mlangoni, naye kwa namna fulani alikuwa ameinamisha kichwa chake, kasema *alimbusu* busu la kwaheri, akatoka nje ya lango, akampungia mkono wa kwaheri tena.

²¹⁴ Akaanza kuteremka mtaani, ndipo ikawa aliwazia, “Vipi kama angekufa? Vipi kama jambo fulani lingenipata? Yeye ndiye mwanamke mpendwa sana duniani. Jinsi ninavyompenda! Ninakumbuka nilipomwahidi madhabahuni nitaishi mwaminifu kwake. Mambo haya yote hapa, daima ningempenda, nimheshimu, na kumthamini. Loo,” akasema, “Mungu akaanza kuhusika na moyo wangu. Nikarudi nyuma, kupitia langoni, nikaingia mlangoni, nikafungua mlango, na kusema, ‘Faye, uko wapi?’” Kasema, “Ninasikia kitu fulani kikifanya, ‘*Huff, huff,*’” mnajua jinsi mwanamke anavyoweza kufanya, mnajua, “amesimama nyuma ya mlango, kidogo analia.”

Kasema alimwangelia namna hiyo, akakivuta kidevu chake, na kumpa busu kubwa midomoni, akageuka, akasema, “Kwaheri.”

Kasema, “Kwaheri.”

Kasema alikimbia nje ya lango, akaangalia kote tena, na kasema aliangalia nyuma, amesimama mlangoni, naye akasema, “Kwaheri.”

Akasema, “Kwaheri.”

²¹⁵ Kasema, “Alisema tu kama alivyosema mara ya kwanza, lakini mara ya mwisho ilikuwa na hisia ndani yake.” Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu tu ninapenda kupeana mikono, kule kuliko na hisia ndani yake.

²¹⁶ Hivyo ndivyo ninavyopenda dini, amina, mtu aliye na hisia ndani yake, ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, na Roho Mtakatifu amewashuhudia, ya kwamba ninyi ni wana na binti za Mungu. Kitu fulani chenye hisia ndani yake, kitu kinachokufanya ujue kwamba ni halisi, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

²¹⁷ Hapa wakati fulani uliopita huko Florida, nilishuka kwenda kule kumtembelea mvulana huyu mdogo, anayeitwa “Little David.” Aisee, ninaamini ninamwona Ndugu *anayeitwa nani* huko nyuma, Morris, kutoka huko chini maskanini. Hiyo ni kweli? Je, unakumbuka usiku ule maskani yetu ilipokuwa ndogo sana, na ilitubidi kwenda kule, ukumbi wetu wa mikutano, na kubadilishana na Little David? Little David alipata jumba

kubwa la mikutano, nasi tulikuwa na wengi kupita kiasi ukumbini mwetu, kwa hiyo tukabadilishana tu. Naye akaja kule, nasi tukaenda, tukachukua lake.

Nikasema, “David, hebu nikulipe hilo,” ama, Bw. Walker, baba yake.

Kasema, “Usijali, usijali, hilo ni sawa, Ndugu Branham. Endelea.”

²¹⁸ Ndipo Little David akashuka akaenda Florida. Na bila shaka ninii . . . Hilo ni jambo moja kuhusu Wapentekoste, wao, “Ndama anajua zizi lake, bwana wake anajua ninii . . . punda anajua hori, lakini watu wangu hawajui.”

²¹⁹ Walipokuwa na huyo Little David, ambaye angewavuta maelfu ya watu, lakini alitoka kwenye dhehebu lingine, kwa hiyo ilibidi madhehebu hayo mengine yawe na Little David, dhehebu lingine, dhehebu lingine, wote wana akina Little David. Mara Mungu alipotoa karama ya uponyaji, huyo mwingine ilimbidi kuwa nayo, ilibidi dhehebu *hili* liwe nayo, na *lile* ilibidi liwe nayo, na *lile*. Loo, jamani! Kamwe hawaelewi, hivyo tu.

²²⁰ Walimchukua huyo mvulana mdogo, maskini hao baba Wakristo wangemzunguka, na kukiinamisha kichwa chake kidogo, wala hakujiwuna (Maskini mvulana huyo alikuwa mhubiri, si, “Mama, wewe mtoto Yesu uliyezaliwa kwenye Krismasi . . . Ile inayofuata ni ipi Mama?” La, la, maskini mvulana huyo alichukua somo na kulishughulikia kama mhubiri.), na kama wote wangemzunguka, wala wasimwache aingiwe na kiburi kichwani mwake, angewaleta makumi ya maelfu ya watoto wadogo kwa Kristo. Lakini la, kila mmoja ilibidi awe na Little David.

²²¹ Kulikuwako na Bibi Willets na hao wengine kule chini, wakiwa na kila namna ya akina Little David, na kurasa mbili za kuwaorodheshea akina Little David. Kwa hiyo akanionba kama ningeshuka kwenda huko, akazima simu. Basi nikashuka nikaenda kule, nao walikuwa na aina fulani ya mwanamke mwinyi, ama ni kitu gani? Hiyo ni kweli, *mwanamke mwinyi*? Namna fulani ya mwanamke, huyo mwanamke mwinyi, sijui maana yake, bali alikuwa ni mwanamke mashuhuri. Na loo, maelfu walikuwa kote pale kuombewa. Hapo ndipo Ndugu Bosworth alipoingia.

²²² Basi, mtu fulani akanijia, Ndugu Lindsay akanijia, na kusema, “Ndugu Branham,” ninaamini ilikuwa ni Ndugu Lindsay ama Ndugu Moore, mmojawapo, akasema, “Mwanamke mwinyi anataka kukuona.”

Nikasema, “Ati *nani*?”

Kasema, “Mwanamke mwinyi.”

Nikasema, “Mwanamke mwinyi ni nani? Na mwanamke mwinyi ni kitu gani?”

Naye akasema, “Yeye ni mwanamke mashuhuri, *kitu fulani* kikuu, unajua.” Kisha kasema, “Yeye anamiliki shamba hili hapa nje.”

²²³ Nikasema, “Ati nimwone, na kuwaacha maskini watu hawa wagonjwa walale hapa? Na yapata elfu mbili wakijaribu kunijia wapate kuombewa, huku ninaondoka alasiri ya leo, ati nimwone mwanamke ambaye ni mzima na mwenye afya, na kuwaacha maskini watu hao walale hapo?” Nikasema, “La, bwana, nitawaona wagonjwa hawa endapo nitapata wakati wa kumwona mwingine.”

²²⁴ “Loo,” akasema, “lakini Ndugu Branham, atakuwa amesimama mlangoni utakapotoka.” Kasema, “Haitachukua muda wako mwingi, anataka tu kukutana nawe.”

Vema, nikasema, “Sawa.”

²²⁵ Nilipokuwa nikitoka, hapa alisimama mwanamke mkubwa mno amejivika vito mikononi mwake vinavyotosha kumtuma mmishenari kote ulimwenguni mara hamsini akihubiri Injili. Basi huyu hapa anakuja, naye alikuwa na miwani kwenye kijiti, alikuwa ameishikilia namna *hii*, naye akasema, “Halo.” Akasema, “Wewe ni *Daktari* Branham?”

Nikasema, “La mama. La mama.” Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham tu.”

Naye akasema, “*Nimefurahi sana* kukutana nawe,” kisha akainua mkono wake juu namna *hiyo*.

Nikaushika mkono huo mkubwa, mnono, nikauvuta chini, nikasema, “Ulete hapa chini nipate kukujua nitakapokuona tena.” Nikajaribu kumfanya . . .

²²⁶ Loo, nakwambia, ndugu, mimi, loo, kamwe sininii . . . Kuna faida gani kujifanya kile tunachokiita, usemi wa mitaani, “Kujigamba,” wakati wewe si kitu, kwa vyovyote vile? Loo, kama Wamarekani wetu hawawezi kujigamba!

²²⁷ Ndugu Arganbright, nina wazo zuri la kusema yale tuliyoona Uswisi, nikimleta . . . mwanamke huyo, akishuka kule akiwa na vito hivi vyote vya maduka ya malimali, tulikuwa na wakati mzuri mpaka Binti Marekani alipoingia, akakiweka kijibwa manyoya mezani, nami, loo! Inatosha kukuchefua. Sikufurahia sana steki hiyo siku hiyo, Ndugu Arganbright, huko chini Lausanne. Mimi kamwe . . . Inakuchefua tu. Loo, yeye ni Bibi Marekani, zile sigara, hapana shaka daktari alimwambia akae mbali nazo awezavyo, alikuwa ameziweka *hivi*, na fimbo kubwa mno huko nje, akijaribu “kujigamba.” Loo, sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Vipi kuhusu hilo?

²²⁸ Nilikuwa nikipitia kwenye jumba la makumbusho si muda mrefu uliopita, nao walikuwa na makadirio ya mwili wa mtu uliolazwa pale. Nao ulikuwa na karibu chokaa ya kutosha kunyunyizia kiota cha kuku, naye mtu huyo ana uzito wa ratili

mia moja na hamsini, na kalisi na potashi ya kutosha tu. Hata hivyo, ikikadiriwa kwa jumla, mtu mwenye uzito wa ratili mia moja na hamsini, mnajua ana thamani gani? Senti themanini na nne.

²²⁹ Nawe utaweka kofia ya dola ishirini juu ya senti themanini na nne, koti la gharama la dola mia tano juu ya senti themanini na nne, uinue pua yako juu hewani, kama mvua ingenyesha, ingekuzamisha, ukijaribu kufikiri wewe ni *mtu fulani* wakati sivyo ulivyo, wewe si kitu ila senti themanini na nne, hivyo tu.

²³⁰ Loo, jamani, unashuka kwenda kwenye mkahawa, unanunua bakuli la supu, na kungekuwa na buibui ndani yake, ungeushtaki huo mkahawa, halafu utamruhusu ibilisi ashindilie sigara, na tumbaku, na dhambi kooni mwako kuilaani nafsi hiyo ambayo ina thamani ya dunia elfu kumi, na halafu unazungumza juu ya ustaarabu. Loo, jamani! Sisi ni . . . Gurudumu limegeuka nyuma tena, naam, bwana.

²³¹ Wale wavulana waliokuwa wamesimama pale waliuangalia huo, mmoja akamtazama mwingine, kasema, “Jack, hatuna thamani sana, sivyo? Senti themanini na nne.”

Nikasema, “Ngojeni kidogo, enyi wavulana, mna nafsi *humo* ndani yenye thamani ya dunia elfu kumi. Hiyo ni kweli.” Yeye kamwe hakadirii . . .

Wewe ni mavumbi, mavumbini unarudi,
Haikusemwa juu ya nafsi.

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha

Nasi tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Huku akisafiri kwenye bahari kuu ya maisha,
Ndugu mpweke na aliyeharibikiwa meli,
Akiona, atatiwa moyo tena.

²³² Loo, napenda hilo vizuri sana, *Zaburi ya Maisha* ya Longfellow.

²³³ Maskini Mariamu alipokuwa akija pale, nikirudi kwenye somo langu, na maskini mashavu yakiona haya, macho yake, alijua alikuwa karibu na nyumba hiyo, moja kwa moja barabarani, akimshuhudia kila mtu alikuwa anaenda kumpata Mtoto.

²³⁴ Huyu hapa Elisabeti anatoka amevaa maskini shela yake, na kusema, “Mariamu!”

Naye akasema, “Elisabeti!” Nao wakaanza kukumbatiana. Loo, jamani!

Naye akasema, “Nina furaha sana kukuona, Mariamu.”

Akasema, “Naam, nina furaha.”

Akasema, “Kumbe.”

²³⁵ Akasema, “Naam, hiyo ni kweli.” Akasema, “Mimi ni mja mzito.” Akasema, “Mume wangu, Zakaria, ni bubu kabisa,” kasema, “hawezi kuzungumza, alikutana na Malaika.”

Akasema, “Naelewa.” Amina. Alijua hayo yote yalihusu nini.

Akasema, “Lakini unajua, Mariamu?” Akasema, “Nina wasiwasi kidogo.”

Kasema, “Kwa nini?”

Kasema, “Nina miezi sita kama mwanamke, mjamzito, na kamwe hamna uhai bado.” Akasema, “Nina wasiwasi kidogo.”

Nami ninaweza kumwona Mariamu na hayo macho madogo, akasema, “Lakini unajua, nina mimba, pia!”

“Loo, wewe na Yusufu mlifunga ndoa?”

“La, mimi na Yusufu hatujafunga ndoa! La.”

“Mariamu, binamu yangu, ati utamzaa mtoto kabla wewe na Yusufu hamjafunga ndoa?”

“Ndiyo!” Amina.

“Loo, itakuwaje?”

²³⁶ “Roho Mtakatifu atanitia uvuli, tayari amefanya hivyo. Loo, na tumboni mwangu kutakuwa na Mtoto mchanga, Ambaye atakuwa mtoto Imanueli. Naye alisema nitamwita Jina Lake Yesu atakapozaliwa.”

²³⁷ Na mara aliposema, “Yesu,” mtoto Yohana akaanza kupaza sauti na kuruka, akiruka juu chini, kwa nguvu alivyoweza kwenda, juu chini. Loo, jamani! Ndipo Roho Mtakatifu akaja juu ya Elisabeti, naye Yohana, Biblia ilisema, yeye alijazwa na Roho Mtakatifu akiwa tumboni mwa mama yake. Loo, jamani! Naam. Mungu hutimiza Neno Lake.

²³⁸ Basi sikilizeni, iwapo mara ya kwanza ambapo Jina la Yesu liliwahi kunenwa kupitia midomo ya binadamu kulimfanya mtoto aliyekufa afufuke, na kuruka kwa furaha tumboni mwa mama yake, linapaswa kufanya nini kwa kanisa linalodai kuzaliwa mara ya pili kwa Roho? Amina.

²³⁹ Kansa inayoua inawezaje kukaa hapo? Mtoto wa jicho mwuaji unawezaje kupenya? Pepo bubu au kiziwi anawezaje kukufunga wakati “Katika Jina Langu watatoa pepo”? Haleluya!

²⁴⁰ Kamwe usitilie shaka, chukua Neno Lake kama Mariamu alivyofanya, na uanze kushangilia. Mtafanya hivyo? Ninzi mtakaooombewa usiku wa leo, mtafanya hivyo, mara tu Jina la Yesu litakapoitwa juu yenu, je, mtaanza kuruka kwa furaha, mkisema, “Mungu asifiwe, yote yamekwisha sasa. Haleluya! Yote yamekwisha sasa”?

Utoke hapa, na mtu yeyote akisema, “Unajisikiaje?”

“Ajabu, ajabu, mzima na bora sana.”

“Mbona? Unajuaje ya kwamba umeponywa?”

“Mungu alisema hivyo, tosha.”

²⁴¹ Kama walivyomwambia Ibrahimu, “Unajuaje utampata huyo mtoto?”

Kasema, “Ninataka yadi kumi za jicho-ndege, ninataka pini, nataka vijibuti.”

“Ati nini? Mbona, wewe ni mzee, mke wako ni mkongwe.”

“Haileti tofauti yoyote, tutapata mtoto.”

“Unajuaje utampata?”

“Mungu alisema hivyo.”

²⁴² Mwezi wa kwanza ukapita: “Sara, unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti.”

“Nitampata mtoto, kwa vyovyote vile, Mungu alisema hivyo.”

²⁴³ Miaka kumi ikapita, miaka ishirini ikapita, miaka ishirini na mitano ikapita: “Unajisikiaje, Sara?”

“Hakuna tofauti hata kidogo.”

“Mungu asifiwe, tutampata huyo mtoto, kwa vyovyote vile.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Mungu aliposema jambo hilo, hilo latosha.”

²⁴⁴ Ibrahimu aliviita vitu visivyokuwako kana kwamba vilikuwako, kwa sababu aliliamini Neno la Mungu, ambapo Yeye anaweza kutimiza ahadi Yake. Nasi tukiwa wafu katika Kristo, tunachukua Mbegu ya Ibrahimu, nasi ni warithi kulingana na ahadi, wala hatuwezi kumtumainia Mungu kwa dakika kumi na tano. Hatuwezi kumtumaini tangu wakati tunapoondoka hapa, hadi wakati wa kutoka mimbarani, tayari unamtilia shaka. Na sasa Unyakuo unatoka wapi?

²⁴⁵ Uzao wa Ibrahimu, unapozifuata amri za Mungu, na kuamini Neno la Mungu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mungu alituma karama na kadhalika na ametuthibitishia ya kwamba Yeye yu pamoja nasi, tunapokuwekea mikono, amini kwa moyo wako wote, toka jukwaani, “Ni kazi iliyomalizika, Mungu alisema hivyo.” Amina.

²⁴⁶ Kasema, “Umepooza na hata huwezi kusogeza kidole.”

Sema, “Tayari nimeponywa.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo. Mungu alisema hivyo.”

“Ndugu Branham alisema hivyo.”

²⁴⁷ La, kamwe, Mungu alisema hivyo. Mungu alisema hivyo, nalo Neno la Mungu ni kweli, hakuna kitu kingine kinachoweza kulizuia. Mungu atupe akina Mariamu zaidi usiku wa leo, na watu watakaolichukua Neno Lake.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapoomba.

²⁴⁸ Je, kuna mmoja humu jengoni, kabla hatujaanzisha mstari wa maombi, angetaka kusema, “Ndugu Branham, laiti ningalikuwa na Roho wa Mungu ndani yangu, lingenifanya nichukue kila Neno la Mungu na kusema ni kweli. Laiti ningalikuwa na Roho wa Mungu ndani yangu ambaye angenifanya niseme, ‘Mungu alisema hivyo, hakuna lingine’?”

Na kila ahadi katika Kitabu ni yangu,
Kila sura, kila kifungu, kila mstari.
Ninatumainia upendo Wake wa Kiungu,
Kwa maana kila ahadi katika kile Kitabu ni
yangu.

²⁴⁹ Mwaweza kuinua mikono yenu, na kusema, “Niombee, Ndugu Branham?” Mungu awabariki. Loo, jamani! Kote jengoni, ni nzuri mno.

²⁵⁰ Je, yupo mwenye dhambi asiyejua jinsi ya kumwamini, angejasiria kuja hapa? Sasa kumbukeni, mimi si mmoja wa hawa wahubiri wa kusikitisha, wanaoitisha mwito wa madhabahuni. Ninaamini Neno hufanya hivyo, la sivyo ha—halifai kitu, kwa vyovyote vile. Mnaona?

²⁵¹ Ninaamini kama unajua Neno, na unamwamini Bwana Yesu Kristo, utakuja moja kwa moja hapa usiku wa leo, na kuligeukia, kusanyiko hili, na kusema, “Nimeshawishika ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, sasa ninamkubali kama Mwokozi wangu binafsi,” kuna maji mengi hapa chini kwenye ziwa, na Roho Mtakatifu anangojea. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo njia ya kuja. Hiyo ndiyo njia ya kuja.

²⁵² Naam, bwana, kama unaamini, mara unapomwamini na kumkubali kama Mwokozi wako binafsi, simama mbele ya watu na kushuhudia hilo, Yeye alisema, “Upesi hivyo nitalishuhudia mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Hiyo ni kweli.

²⁵³ Utakuja sasa? Tunapongojea kwa muda kidogo tu, huku muziki ukiendelea kucheza.

²⁵⁴ Bwana Yesu, nakuomba Wewe, Bwana, sijui kusanyiko hili, Wewe unalijua, Bwana. Tusaidie, sasa Bwana, kama kuna mmoja hapa, ili kwamba nitakuwa na hakika kwenye ile Siku kuu ya Hukumu kwamba hawatanielekezea ki—kidole kilichokonda, na kusema, “Laiti ungaliita usiku ule.” Ninawapa fursa sasa, Baba, nafsi yao ndiyo iliyo hatarini. Jalia waje, Baba, sasa na kukiri dhambi zao na kumwamini Yesu, Mwanao, wamkubali kama Mwokozi wao binafsi.

²⁵⁵ Yesu yeye yule aliyechukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la Mariamu wakati Yehova, Mungu Mwenyezi, alipomtia uvuli, na kuleta Seli ya Damu tumboni mwake, iliyochanganywa na yai lililokuwa ndani ya mwanamke huyo, akaleta, si damu ya Myahudi, wala damu ya Mmataifa, bali Damu ya Mungu, na kupitia hiyo, Damu takatifu isiyoghoshiwa, hutuokoa na dhambi zetu.

²⁵⁶ Jalia, Bwana, ya kwamba endapo kuna mwenye dhambi, Wewe unaujua moyo wao, sijui, jalia waje sasa wakati tunapongojea.

Unapozuru wengine,
Usinipite.

Mwokozi . . .

Nisipowaona tena, hii hapa nafasi yako.

. . . kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Nataka kuutafuta uso Wako;
Ponya ninii yangu iliyojeruhiwa,
iliyovunjika . . .

[Ndugu Branham anawaombea wale walio madhabahuni, maneno yake hayatambuliki—Mh.] . . . ? . . .

²⁵⁷ Mtu huyu, mwanamke huyu, na mvulana huyu wa Kihindi, watu watatu wa thamani, tunao ushindi sasa. Wamekuja hapa juu usiku wa leo, kwa sababu Mungu aliwaita.

²⁵⁸ Sasa, Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipoitwa na Baba Yangu kwanza.” Hiyo ni kweli? “Baba yangu hana budi kumwita kwanza. Na wote wanijiao Mimi, sitawatupa nje kamwe, na nitampa Uzima wa milele, na nitamfufua katika siku ya mwisho.” Je, hivyo ndivyo Mungu alivyosema? Hiyo ni ahadi Yake.

²⁵⁹ “Sasa, yeye anioneaye aibu mbele za wa—watu, nitamwonea aibu mbele Zake kwenye Hukumu, Baba, na Malaika watakatifu, bali yeye atakayesimama na kunikiri mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

²⁶⁰ Majina haya ambayo nimepewa sasa hivi, Mungu ameyaandika katika Kitabu cha Uzima. “Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Mnaamini hilo?

²⁶¹ Sasa, hawa marafiki zangu, marafiki zako si hivyo tena, wao ni ndugu na dada katika Kristo Yesu.

²⁶² Kama kuna baadhi ya wahudumu hapa, wa mahali hapa, wanaowajua watu hawa, ninawatakeni mje mbele sasa, mhudumu yeyote aliye katika mahali ambapo watu hawa

wanaishi, aje na kuwapa mkono wa kuume wa ushirika, na kuwapeleka kanisani mwenu, na kutekeleza maagizo waliyopewa katika Biblia. Kuna mchungaji hapa ambaye—ambaye uko kwenye moja ya makanisa yanayowajua hao watu?

²⁶³ Je, ninyi watu ni wenyeji hapa, katika jamii hii, mahali popote kupitia hapa? Hamtoki hapa. Vema, hawatoki kwenye maeneo haya hapa, basi. Hivi wewe, nanii, ndugu yangu mvulana wa Kihindi, wewe pia hutoki hapa?

²⁶⁴ Ni wangapi wenu mnaowakaribisha katika Ufalme wa Mungu kama ndugu na dada? Inueni mikono yenu. Mungu awabariki. Unaporudi sasa nyumbani kwako, je, utaenda kwenye kanisa zuri na kumwambia mchungaji ya kwamba umeokoka? Utafanya hivyo? Utafanya hivyo? Utafanya hivyo, bwana? Utafanya hivyo, dada? Mungu awabariki. Loo, hilo ni sawa.

²⁶⁵ Hebu tuimbe *Kibarikiwe Kifungo Kifungacho* sasa kwa ajili yao, wanapoenda kwenye viti vyao.

²⁶⁶ Nendeni sasa, na kama sitawaona tena ng'ambo hii ya mto, nitawaona Kule. Wanapopita, wapeni mikono.

Kibarikiwe kifungo . . .

[Ndugu Branham anazungumza na wale madhabahuni ambao ndio kwanza waukubali wokovu, mengi ya maneno yake hayatambuliki. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . .

²⁶⁷ Loo, hilo linanifanya tu nijisikie vizuri sana. Wazia tu, hiyo ni kusema, ya kwamba papo hapo pana thamani ya dunia elfu thelathini kulingana na Biblia, kila nafsi ina thamani ya dunia elfu kumi. Loo, Yeye si ni wa ajabu?

²⁶⁸ Ninaamini Mungu atamwita mvulana huyo wa Kihindi kuwa mhubiri.

²⁶⁹ Mama huyo alisema alitoka Hot Springs, Arkansas. Na nilipokuwa kule mkutanoni, nikiwa na wakati mgumu kama uliwahi kuwako, yeye alisema Nuru hiyo (Ni wangapi walioiona picha Yake, sasa? Tunayo hapa, nadhani ninyi nyote mmeipitia.), Nuru hiyo, aliiona ikija juu yangu nilipokuwa nikihubiri huko, ndipo mumewe akasema amerukwa na akili, hakuiona. Yeye aliiona! Nayo ikadumu naye hata sasa, amekuwa Mkristo sasa. Mungu akubariki, dada.

²⁷⁰ Nuru iyo hiyo ya neema ya Mungu iko juu yenu sasa, itawaongoza hadi kwenye Nchi ya Ahadi, hilo ndilo ililotumiwa. Amina. Amina.

²⁷¹ Vema, Billy Paul yuko wapi? Uligawa kadi zipi za maombi? Mahali fulani. . . Yuko hapa? C, hamsini hadi mia moja. Vema. Ni nani aliye na C, hamsini? Inua mkono wako, ili tuwe na hakika ya kuwaingiza wote ndani, tutawaita. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

272 Mnataka niwaambieni jambo fulani? Kuna watu fulani hapa ndani usiku wa leo walio na imani, hii ndiyo imani bora zaidi niliyopata tangu mkutano ulipoanza. Ninaweza kuona maono yakitokea juu ya watu papa hapa sasa. “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.” Kuwa tu na imani, wala usiwe na shaka. Yeye ni wa ajabu, siyvo?

273 Mnamwona huyu mzee aliyeketi hapa? Anaugua ugonjwa wa kukakamaa kwa ateri, na yuna shida kidogo ya kusikia. Kama ungeamini hapo, bwana, kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Amina.

274 Huyu hapa mwanamke ameketi papa hapa akimwombea binti yake, hayupo hapa, aliye na ugonjwa wa mapindi. Kama unaamini kwa moyo wako wote, mama! Ulingusa Yeye. Unaona? Mwamini Mungu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

275 . . . shida ya kibofu nyongo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Mwanamume aliyeketi karibu naye mwenye ugonjwa wa moyo, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Itatendeka. Likubalini, nyote wawili. Mna kadi za maombi? Hamna? Si lazima mwe nayo. Mnaona? Anaujua moyo wako, hilo ndilo ulilokuwa ukiombea. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kusudi kusanyiko liona kwamba ni kweli. Inua mkono wako. Vema, papa hapa.

276 Mnaona jinsi ilivyo? Roho Mtakatifu yupo hapa, inakubidi tu kumwamini. Hiyo ni kweli? “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana kama unaweza kuamini.”

277 Ninaangalia upambanuzi. Hebu mstari wa upambanuzi uwe huko nje. Nitawaombea tu hawa. Ninaona jambo fulani likitukia. Amina.

278 Ugonjwa wa tumbo umekwisha, bwana, unaweza tu kuacha kuomba hapo. Amini Bwana alikuponya. Mungu akubariki. Unaamini? Ulikuwa unaomba, “Bwana, jalia aseme nami tafadhali usiku wa leo, sina njia ya kufika kule.” Ugonjwa wako wa tumbo umekwisha, nenda nyumbani, upate afya sasa, Yesu Kristo anakuponya.

Aliyeketi hapo akiomba kwa bidii tu awezavyo, nami nimeiona ile Nuru ikizunguka juu yake namna hiyo, namwona akikataa chakula.

Uko sawa sasa. Nenda, ukaponywe. Um-hum.

279 Ninamwona mwanamke ameketi hapa, ameshika kadi yake ya maombi mkononi mwake, ameketi papo hapo. Nina shaka kama ananisikia, ana shida ya kusikia, bali kama angekubali tu uponyaji wake, iko moja kwa moja juu yake sasa hivi. Ana damu mbaya, pia, ni ugonjwa wa ateri mikononi mwake, na kadhalika. Hiyo ni kweli, huyu mama mzee, nywele fupi zilizokatwa, amevaa nguo ya kijani kibichi, ameshika kadi mkononi mwake.

280 Kama utaamini sasa hivi, hata haitakubidi kuja jukwaani. Mnaweza kunisikia? Vema! Hilo lilitosha. Amina. Hilo ni sawa. Haikubidi kuja sasa, mwambie tu haimlazimu kuja. Mwambieni, mtu fulani hapo, si lazima aje. Uko sawa. Mungu akubariki.

281 Loo, Bwana asifiwe! Ninapenda kuona hilo. Maskini mwanamke mkongwe, aliyeketi hapo, hakuna mtu anayemwalia, hakuna mtu anayemjali, lakini Mungu alimwona. Amina.

282 Huyu ndugu aliyeketi hapo ameinua kichwa chake hewani, akiomba tu, huna kadi ya maombi, sivyo, bwana, huko nje? La, huihitaji, uko sawa, kwa vyovyote vile. Nenda nyumbani, utapona.

283 Sasa, Yeye angali hapa? Waligusa nini? Pindo la vazi Lake. Hawakunigusa, walimusa Yeye. Sasa mnaona, imani yao iliwaokoa. Je, hilo linamfanya Yesu Kristo, Yule tuliye kuwa tukinena habari zake, aliyezaliwa na bikira...? Yeye hajafa, Yu hai. Hiyo ni kweli?

284 Unasema, “Ndugu Branham, unafanyaje hilo?”

285 Ni karama tu. Unajiachilia tu mbele za Mungu, na... Kama tu maikrofoni hii, ambayo ni—ambayo ni bubu. Maikrofoni hiyo haiwezi kuzungumza yenyewe, wala na mimi siwezi kuzungumza.

286 Ninakujaaje? Kila mtu niliyemwambia lolote muda mfupi tu uliopita, yeyote yule, inua mkono wako endapo hatufahamiani. Kila mtu ambaye ndio kwanza aitwe, Roho Mtakatifu aliita, inueni mikono yenu kama... Haya basi. Mnaona? Hao hapo aliowaita, wala simjui hata mmoja wao.

287 Ni wangapi kwenye mstari huu nisiowajua? Inueni mikono yenu, mnajua ya kwamba hatufahamiani, sisi kwa sisi. Simjui hata mmoja wao. Mnaona? Kwa hiyo, ningekuwa bubu, ni Roho Mtakatifu akinena kupitia hapa.

288 Sasa, Mungu anaweza kumtumia mwanadamu kama maikrofoni Yake. Hivi hamwoni hivyo? Kama wewe mwenyewe unaweza tu kuwa bubu vya kutosha, uache Mungu alifanye. Hiyo ni kweli, hiyo ndiyo njia. Amina.

289 Vema. Hiyo ina...? Kuna mtu ameingia? Yeyote kati ya hao wengine tisini, ama kutoka mia moja? Vema. Hebu tuanzishe mstari wa maombi. Tutangojea mpaka tutakapowamaliza hawa. Mnaona?

290 Sasa kumbukeni, katika mstari wa maombi, mumeona upambanuzi, hao huko nje wasio na kadi ya maombi. Sivyo? Mnaamini hiyo inafanya upako, juu yangu sasa, wa Roho Mtakatifu? Je, Biblia inasema hivi (Je, Neno la Mungu ni kweli?), “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya”? Hiyo ni kweli?

²⁹¹ Sasa angalieni, muda mfupi uliopita wakati Roho Mtakatifu alipokuwa akishuka, hizo zilikuwa ni *baraka* za Bwana, sasa, hizi mnazoonza zikitenda kazi namna hii ni *nguvu* za Bwana. Hizo ni baraka; usichanganye baraka na nguvu. Unaweza kuwa na baraka, wala usiwe na nguvu za kutosha kuponya maumivu ya jino. Lakini nguvu za Bwana ni kumdhihirisha Mungu. Mnaona ninalomaanisha? *Nguvu* za Bwana. Sasa, sasa, hao walikuwa ni watu huko nje ambao hawana kadi ya maombi. Sasa huyu hapa mmoja aliye na kadi ya maombi.

²⁹² Wewe—wewe ni—wewe ndiye yule mama aliye kwenye mstari wa maombi? Vema, njoo hapa na usimame papa hapa mbele yangu. Niangalie. Ninasema kwamba kama vile Petro na Yohana walivyopitia kwenye lango liitwalo Zuri. Sasa, sijawahi kukuona maishani mwangu, hatufahamiani. Mungu anatumia sote wawili. Kama Mungu ata—ataniambia kilichokuleta hapa, utaamini mimi ni nabii Wake? Utaamini.

²⁹³ Ni wangapi wenu nyinyi wengine huko nje mtaamini? Angalieni hapa, huu *hapa* mkono wangu, hii *hapa* Biblia ya Mungu: Nijuvaye mimi, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, huenda nilikuwa nikishuka mtaani, mahali fulani, hapa nje, nikamwona akipita, ama kwenye motokaa yake, kama mimi. . . Ninamaanisha kumjua. Anasema kwamba hanijui; simjui.

Kama hiyo. . . Hiyo ni kweli, mama? Ikiwa ni kweli, inua tu mkono wako, ili watu waone.

²⁹⁴ Sisi hapa. Sasa, nguvu za Mungu ni nini? Ishara ya Yesu Kristo ni nini? Yesu alisema, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Hiyo ni kweli? Naye alisema nini katika Yohana Mtakatifu 5:19? “Sifanyi lolote mpaka Baba anionyeshe.”

²⁹⁵ Sasa, katika Biblia wakati Filipo alipomjia, Yeye alijua ya kwamba alikuwa amemwona Nathanaeli chini ya mti; akamwambia yule mwanamke kisimani shida yake ilikuwa ni nini; mwanamke aligusa vazi Lake kwenye kusanyiko, akaenda huko nje, akamwambia; Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu; Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

²⁹⁶ Nayo Biblia ilisema ya kwamba Neno, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno,” (Ni wangapi wanaojua hilo?) “huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Hiyo ni kweli?

²⁹⁷ Sasa, hebu niwashike, Waebrania 4, Biblia ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wowote ukatao kuwili, likichoma hata kugawanya mifupa na mafuta yaliyomo ndani yake, tena ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Yesu alitambua mawazo yao, kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Hiyo ni kweli?

298 Sasa, Mungu aliwatumia wanadamu kama mawakala Wake. Hiyo ni kweli? Daima, Mungu alimtumia mwanadamu kuwa wakala Wake, Yesu alikuwa ni Wakala wa Mungu, Eliya alikuwa ni wakala wa Mungu, Yohana alikuwa ni wakala wa Mungu. Sasa, kama wakati huu Mungu ana shahidi, “Bwana, jalia niwe wakala Wako.” Basi hebu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

299 . . . ana shida gani. Acheni awe mwamuzi kama ni kweli ama si kweli. Hilo linapaswa kutatuliwa na kusanyiko. Hiyo ni kweli?

300 Angalia huku, dada. Sasa, kama ninaweza kujistarehesha. . . Niamini tu, kama vile Petro na Yohana walivyosema, “Tutazame sisi.” Mnajua ninalomaanisha? Sikilizeni tu yale ninayosema. Sikujui, sijawahi kukuona, hatufahamiani kabisa, kama Mungu ataniambia hali yako, utajua kama ni kweli ama si kweli. Basi itakusaidia? Itakusaidia? Isingekuponya, bali itakusaidia kuwa na imani ya kuponywa, kama wewe ni mgonjwa. Sijui kwamba wewe ni mgonjwa, si—sininii chochote kukuhusu, sijawahi kukuona.

301 Lakini uko hapa kwa sababu una shida shingoni mwako; ni kivimbe shingoni mwako. Halafu basi, ninaamini daktari ametaja kitu *fulani* kingine kilicho shida na. . . katika ninii—katika ninii. . . La, ni mate, tezi ya mate. Hiyo ni kweli. Vema, Bibi Rogers, hilo ndilo jina lako. Sasa, utarudi nyumbani kwako ukiwa na furaha, kwa sababu utakuwa mzima. . . ? . . .

302 Vema. Unaamini kwa moyo wako wote? Vema, basi iweni na imani tunapowaombea watu. Nyote nisaidieni sasa. Hayo maono tayari yamenifanya dhaifu. Mnaona, siwezi. . . Ni wangapi wanaojua ya kwamba maono hukudhoofisha? Musa aliposhuka, hakuweka ninii yake. . .

303 Ninazungumza kwa dakika moja tu ili kurejesha nguvu zangu tena sasa. Unaona? Unaenda mahali pengine, uko katika ulimwengu mwingine. Mnaona yaliyotukia, yanayotendeka: Yaliyokuwako, yaliyoko, na yatakayokuwako. Mnaona? Musa alifanya muujiza huo wakati mmoja nao Israeli wote wakamwamini.

304 Mimi ni ndugu yenu ambaye Yesu Kristo alimtuma, nikashuhudiwa na Nuru iliyokuwa juu yangu miaka mingi iliyopita. Hata nilipozaliwa, kama mvulana mdogo, kwenye umri wa miaka ishirini na mmoja nilifanyika mhudumu, Yeye alithibitisha huko chini mtoni mbele ya watu elfu kumi, ilisambazwa kwenye vyombo vya habari vya Associated.

305 “Nilikuja kwako, na kukwambia juu ya kuwawekea watu mikono, na kuona karama ikitenda kazi, nilikwambia kwamba itakuwa kwamba utajua siri za moyo.” Kila kitu ni jinsi hasa Yeye alivyosema, na kimetabiriwa kimetimia. Hiyo ni kweli? Wote waliokuwa katika huduma yangu ya kwanza, inueni mikono yenu kama hayo yalitabiriwa yangetimia.

306 Biblia ilisema, “Akiwepo mtu miongoni mwenu anayedai kuwa ni nabii ama wa kiroho, na yale asemayo yanatimia, msikieni kwa kuwa niko pamoja naye.” Hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo ishara yake.

307 Baadhi yao wanasema, “Vema, Ndugu Branham,” hapa si muda mrefu uliopita, mtu fulani alisema, “Ndugu Branham—Ndugu Branham ni sawa wakati anapopambanua, lakini theolojia yake si sahihi.”

308 Sasa, hilo linakuonyesha tu unajua kiasi gani maana ya nabii. Sijiti mwenyewe nabii, ninyi mnaniita. “Neno la Bwana lilimjia nabii.” *Nabii* ni nini? Ni shahidi wa kutabiri, kuonyesha thibitisho ya kwamba yeye ni mfunuzi wa Neno la Kiungu. “Neno la Mungu lilimjia nabii.” Angalia hilo chini uone hilo si sahihi.

309 Sasa, kwenu mnaosimama kwenye mstari wa maombi, tutawawekea tu mikonu sasa. Mnayuka, kusudi nimpate kila moja wenu. Na kuna kadi zingine. Ninaamini mtu mwingine huko nje ana kadi, sivyo? Kuna zingine tulizochukua ambazo zimebaki nyuma? Ninaamini kutoka za A au za B. Kadi moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, saba zimesalia. Vema, tutawawekea moja kwa moja mwishoni mwa mstari huu, tuwapitishe moja kwa moja.

310 Lakini sasa, tunapoanza kuomba, ni wangapi huko nje, kwa kusanyiko hili, utainua mkono wako kwamba utakuwa unawaomba watu hawa, pia? Ninyi nyote, ninyi nyote ombeni sasa. Tunataka... Vipi kama huyu alikuwa ni dada yangu? Mbona, ni dada wa mtu fulani, binti wa mtu fulani, mtoto wa mtu fulani. Na tuombe sasa, ninyi nyote huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

Sasa njoo, dada.

311 Baba uliye Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, lile Jina lililomfanya mtoto Yohana afufuke kutoka kwa wafu, aruke tumboni mwa mama yake, naomba limponye dada yetu. Amina. Vema.

Njoo, bwana. Mwamini sasa kwa moyo wako wote. Njoo. Unaamini?

Ee Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye mtu huyu wa thamani. Amina.

312 Sasa, unajua ninajua shida yako, bali haifai kitu kuwaambia, maana mnajua shida ni nini, sivyo? Lakini unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, hata hivyo? Basi maskini kikohozi hicho kitakuacha, na pumu itatoweka, utaendelea, upate afya.

Vema, njoo ukiamini sasa.

313 Baba yetu wa Mbinguni, ninambariki dada yangu, na kuitia juu yake Jina hilo, ambalo lilimfanya mtoto Yohana kuruka

ndani ya tumbo la mama yake. Tujalie, Bwana, kwa ajili ya uponyaji. Amina.

Mungu akubariki, dada.

Njoo sasa. Unaamini kwa moyo wako wote? Unajua ya kwamba ninajua shida yako.

Ee Bwana, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, ninapoweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda, ukifurahi sasa, ukiwa na furaha.

Sasa, ndugu, unaamini Yeye atafanya hivyo?

³¹⁴ Katika Jina la Yesu Kristo, kwa kuwa Jina hilo, litoshelezalo kwa yote, “Katika Jina Langu, watatoa pepo,” hii *hapa* mikono yangu, “wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya, ishara hizi zitafuatana na mwaminio.” Bwana, umethibitisha ya kwamba ninakuumini, kwa hiyo ninamwombea, katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda kwa furaha, shida yako imekwisha.

Unaamini, dada?

³¹⁵ Bwana Mungu, katika Jina la Yesu, ninaweka mikono juu ya dada yangu, mimi ni mwaminio, ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao,” jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Njoo, dada, mwamini kwa moyo wako wote.

³¹⁶ Sasa, Baba Mungu, kama mwaminio, pamoja na kanisa hili kuu la Mungu hapa usiku wa leo, tukiweka mikono juu ya dada yetu, na kuuhukumu ugonjwa huo, na kuomba uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

³¹⁷ “Maombi ya imani yatamwokoia mgonjwa yule, Mungu atamwinua.”

³¹⁸ Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mkono wangu juu ya dada yangu, na kuomba kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba Wewe utamponya, na kumpa afya. Jalia aende akaponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda tu ukifurahi vile, ukishangilia, yote yamekwisha.

³¹⁹ Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yangu aponywe sasa. Ninamwombea, kupitia Jina hilo litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu. Amina.

Nenda, ukishangilia ukisema, “Asante, Bwana.”

³²⁰ Sasa, kile ambacho sielewi ni kwa nini usishangilie na kumsifu Mungu unapopita? Sasa, hilo ndilo silielewi, enyi kanisa. Hivi hamjui ya kwamba Mungu ni Mungu tu wakati mmoja kama alivyo mwingine? Mnaona?

³²¹ Sasa, mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Sielewi.”

³²² Vema sasa, sikilizeni, mnajua siwakemei, sivyo? Mnajua ninajaribu kuwaletea ukweli. Mnaamini hilo? Mnatambua jambo hilo. Mungu, mimi. . . Hakukuwako na mmoja aliyepita pasipo mimi kuona shida yao. Kama nikianza kwenye ono, linafanya nini? Linawatawanya tu, na haya—haya basi. Mnaona? Watu watapita, watapitia hapa, na kusema, “Naam, naam,” na unalipata. Unaona? “Vema, la, sikulipata kamwe.” Hiyo ndiyo sababu mnasambaza kadi za maombi, msipofanya hivyo, watarudi moja kwa moja mstarini tena, watarudi tena, inadhoofisha tu imani yako kila wakati, inakuwa dhaifu zaidi na zaidi, zaidi na zaidi.

³²³ Mara tu unapopitia hapa, kana kwamba unapita chini ya msalaba. Hupiti karibu nami, unapita karibu na Yeye. Anakujua, anajua yote kukuhusu, angeweza kusema chochote alichotaka kusema. Mnaamini hilo?

³²⁴ Hapa, wewe mama, hatufahamiani, Mungu anakujua. Unaamini Yeye anaweza kuniambia shida yako ni nini? Kama angekwambia, ingekusaidia? Unamwombea mtu mwingine, hiyo ni kweli, mume wako. Mumeo ana matatizo ya ndani, ana ugonjwa mbaya sana wa kichwa. Yeye ni shujaa wa vita, aliumizwa vitani, anaumwa sana na kichwa. Umetoka mahali panapoitwa Fort. . . ? . . . jina lako ni Bibi O’Neil. Chukua lesio hiyo ukaweke juu yake. Naye. . . Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka. Kivuli cheusi kimentia uvuli. Nenda, amini sasa, dada, na uwe. . . ataponywa katika Jina la Yesu.

Sasa, unaamini? Amini. Sasa mnaona, karibu inaniua.

Njoo ukiamini, bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Njoo.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. . . ? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Njoo, ndugu.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. . . ? . . .

³²⁵ Sasa, unaamini? Unaamini Mungu ataniambia kuhusu uponyaji wako? Uvimbe, hiyo ni kweli. Mnajua jinsi nilivyogundua hilo? Angalieni *hapa*. Sasa, naweka mkono wangu juu ya wako. Unaona jinsi umevimba na kugeuka ukawa mwekundu? Unaona vitu hivyo vidogo vyeupe vikipita juu yake? Hiyo inaonyesha ya kwamba ugonjwa wako ni uvimbe. Unafaa kufanyiwa upasuaji. Unaamini? Sasa angalia, hebu nikuonyeshe mkono wangu mwingine. Unaona? Haviko mkononi mwangu *hapo*. Sasa weka *huu* nyuma *kule*. Hivyo hapo.

³²⁶ Sasa, kwenu ninyi watu wa zamani, mnaona hilo? Hiyo ni kweli kabisa. Sasa angalieni. Unaniamini kwa moyo wako wote?

327 Ninaweza kuufanya ukuache, bali siwezi kuuzuia usirudi. Sasa, ili upate kufahamu kabisa, chukua mkono huu mwingine *hapa*, weka mkono wako *hapa*. Sasa mkono wangu unaonekana wa kawaida tu, sivyo? Huo ni mkono wako wa kushoto. Sasa chukua mkono wako. Sasa weka mkono *huu* juu yake. Huo hapo, hauonekani wa kawaida *hapo* sivyo? Sasa ninaweka wangu juu yake, ungali ni wa kawaida. Weka wako juu yake, huo hapo. Unavimba, unakuwa mweusi mwekundu, vitu vidogo vyeupe vikitiririka juu yake, vikifanya, “*Whirrrr, whirrrr.*”

328 Huo ni ule uvimbe. Unaona, ni kuongezeka kwa seli zilizo hai mle ndani, kitu fulani cha kukuua. Ninaweza kuufanya uondoke, kama utaamini, hautarudi. Vema, angalia mkono wangu.

329 Afadhali uinamishe kichwa chako kwa hili, huku ni kufukuza kitu fulani.

330 Ee Bwana, yasikie maombi ya mtumishi wako, yajibu maombi yangu, Baba.

331 Uvimbe, ewe ibilisi, mwache mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yake!

332 Huyu hapo anaenda. Sasa, dada, sasa angalieni mkono wangu. Wote umeondoka sasa, sivyo? Uvimbe umekufa. Nenda zako ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.”

333 Kuna mtu aliyewahi kuona hilo likifanywa hapo awali? Mnaona, Mungu kamwe hachukui karama. Hapa, mwangalieni mwanamke huyu hapa.

334 Nipe mkono wako. Unauona? Naam, bwana, ugonjwa wa tumbo, unao tumboni mwako. Angalia mkono wangu hapa. Unaona jinsi unavyovimba? Angalia, sasa ondoa mkono wako. Unaona ukirudi kawaida? Sasa ninaweka mkono wangu juu ya wako. Haliusumbui. Sasa chukua mkono wako mwingine. Haliusumbui. Sasa, chukua mkono *huu*, uuweke *pale*. Hicho *hapo* kidonda chako. Unakiona *hapo*? Vema. Sasa utaamini kama nikikiondoa kwako kwa maombi, utaamini kitakuacha, utaenda zako, na kula chakula chako cha jioni, na upate afya?

335 Bwana Mungu, ninampa changamoto ibilisi huyu si kwa miujiza, lakini huu ndio usiku wa mwisho wa ibada. Ili watu wapate kujua ya kwamba Wewe ni Mungu, litukuze Jina Lako miongoni mwao, Bwana.

336 Shetani, mwache mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo!

337 Huyu hapo akiondoka. Sasa angalia mkono wangu. Sasa weka mkono wako mwingine juu yake. Unaona jinsi ulivyo kawaida? Sasa rudisha mkono uo huo, na umeona yaliyotukia muda mfupi uliopita, sasa rudisha mkono huo, haya basi. Sasa ugonjwa wako wa tumbo umepona, nenda zako ukishangilia.

338 Iweni tu na imani, hivyo tu. Mnaona? Karama zote hufanya kazi. Naye aliniambia hivi majuzi, “Nena tu Neno,

nalo litatendeka kama utawafanya watu wakuamini.” Sasa, ni wangapi waliowahi kusoma kitabu changu? Malaika wa Bwana aliniambia, “Utapewa . . .”

Nikasema, “Hao watu hawataniamini.”

³³⁹ Akasema, “Utapewa ishara mbili: Moja, utashika mkono wao na kuwaambia wana shida gani. Wasipoamini hilo, basi utawaambia siri yenyewe ya moyo wao, nao itawabidi kuamini hilo.”

³⁴⁰ Ndugu mhubiri kutoka huko chini, hivi wewe . . . ? Si hivyo ndivyo ilivyokuwa nilipokuwa kwenye mkutano wenu? Hii hapa, yote mle ndani. Sasa, Mungu alisema, “Sema tu Neno, waombe wagonjwa, itatukia.” Haina budi kutukia.

Katika Jina la Yesu, mponye mtu huyu, Bwana. Amina.

Nenda ukiamini sasa, bwana. Akufanye . . . kupona . . . kwa moyo wako wote.

Ulikuwa hapa muda mfupi uliopita kwa ajili ya wokovu.

Sasa, Bwana, mponye, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Yeye ni mtoto Wako.

Amini sasa.

Njoo, dada. Ugonjwa huo wa mgongo utakuacha. Nenda zako, ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.”

Njoo.

Katika Jina la Bwana Yesu, mponye ndugu yangu. Tujalie, Bwana. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu. Tujalie, Bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia Roho Mtakatifu anayetia mafuta sasa, amponye ndugu yangu. Amina.

Mungu akubariki, kipenzi.

Katika Jina la Yesu Kristo, msichana huyu na aponywe. Amina.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia nguvu za Shetani zimwache mwanamke huyu. Amina.

Hivi hamwamini vivyo hivyo sasa kwa ajili yao, kama mnavyoamini kwa ajili ya wengine? Hakika, mnaweza kuamini.

³⁴¹ Kama nikikwambia shida yako, itakusaidia? Vema. Ni mgongo wako na miguu yako, ni mshipa uliobanwa. Una mtu fulani moyoni mwako unayemwombea, ni rafiki aliyepooza. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa, je, ilikusaidia? Nenda ukiamini. Amina.

Unaona, kuwa tu na imani, amini.

Katika Jina la Yesu, uponywe. Amina.

Kuwa tu na imani, usiwe na shaka.
 Katika Jina la Bwana Yesu, uponywe.
 Njoo, dada, ukiamini.
 Katika Jina la Yesu, uponywe.
 Njoo, dada, ukiamini kwa moyo wako wote.
 Katika Jina la Bwana Yesu, uponywe.

³⁴² Hivi hamwezi kuelewa ya kwamba ni Roho Mtakatifu anayesema hivyo?

Katika Jina la Bwana Yesu, uponywe.
 Njoo, dada, amini sasa.
 Katika Jina la Bwana Yesu, uponywe.

Unaamini hilo? Ulikuacha papo hapo. Sasa, dada, kama wote wangukuwa na imani kama hiyo, ingekuwa ni sawa. Uko huru sasa, nenda.

³⁴³ Njoo, bwana. Angalia, ulikuwa umeketi pale muda mfupi uliopita ukishangilia nilipokuwa nikihubiri. Hiyo ni kweli. Nilikuona huko nyuma, ono lilikuja niliposema muda mfupi uliopita, “Laiti wangukuwa tu na imani kiasi hiki,” ilikuwa juu yako. Unaugua ugonjwa wa mgongo, unaugua ugonjwa wa kifua, una shida miguuni mwako, ilisababishwa na kuanguka vibaya kulikokupata. Uliponywa kabla ya kuja mstarini. Nenda zako, na ushangilie na ufurahi, katika Jina la Yesu.

Njoo, dada, amini.
 Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

Nenda ukishangilia sasa, usiwe na shaka, amini tu sasa. Vema. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . lakini amefaulu. Unaamini ataponywa?

³⁴⁴ Ninalaani pepo huyu ambaye amemfanyia huyu dada uovu huu! Jalia aondoke hapa, usiku wa leo, na awe mwanamke mwenye afya kushuhudia kwa utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba aondoke! Amina.

³⁴⁵ Sasa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Simameni kwa miguu yenu kila mmoja wenu, na mumpe Mungu sifa.

³⁴⁶ Ee Bwana Mungu, waponye watu hawa ambao lesa hizi zinawawakilisha, waponye wasikilizaji hapa. Jalia Shetani asiweze kumfanya mmoja wao kutilia shaka, lakini jalia kila mmoja wao aponywe kabisa.

³⁴⁷ Toka hapa, Shetani! Ninakupa changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba uondoe mikono yako kutoka kwa watu hawa! 

60-0724 Neno La Mungu Lisilobadilika
Lake County Fairgrounds
Lakeport, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org